BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

FEBRUARI, 2025

YALIYOMO **UK**

1) SEHEMU YA KWANZA - UTANGULIZI …….. ……..3

2) SEHEMU YA PILI - MAUDHUI ……7

A) WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA UCHUKUZI ……..7

B) WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI ……30

C) WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI ……39

3) SEHEMU YA TATU – HITIMISHO ……60

RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

SEHEMU YA KWANZA - UTANGULIZI

1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu cha 85 ya mwaka 1984 na Kanuni ya 119 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, (Toleo la 2024).

Majukumu ya Kamati hii yameorodheshwa kwenye Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

a) Kufatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
b) Kufatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Wizara ilizotoa katika Baraza;
c) Kufatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika;
d) Kuchunguza na kufatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;
f) Kushughulikia miswada ya sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;
g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo;
h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati mbali ya majukumu yake yaliyoainishwa kwa mujibu wa Kanuni pia ina jukumu la kufatilia utekelezaji wa wizara tatu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwemo Mashirika, Mamlaka na Vitengo vilivyomo ndani ya Wizara hizo. Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii ni: -

1) Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi
2) Wizara Ardhi na Maendeleo ya Makaazi
3) Wizara ya Maji, Nishati na Madini

1:1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati imeundwa na Wajumbe wanane (8) na makatibu watatu (3) kama ifuatavyo:-

Nam	**Jina**	**Wadhifa**
1.	Mhe. Yahya Rashid Abdalla	Mwenyekiti
2.	Mhe. Aza Januari Joseph	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Ameir Abdallah Ameir	Mjumbe
4.	Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Mjumbe
5.	Mhe. Hassan Hamad Omar	Mjumbe
6.	Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir	Mjumbe
7.	Mhe. Mwanajuma Kassim Makame	Mjumbe
8.	Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed	Mjumbe
9.	Mhe. Simai Mohammed Said	Mjumbe
10.	Ndg. Himid Haji Choko	Katibu
11.	Ndg. Salma Muhsin Haji	Katibu
12.	Ndg. Saad Othman Saad	Katibu

1:2 MALENGO YA KAMATI

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ilifanya kazi zake kwa kufata malengo yafuatayo:

1) Kufatilia maagizo yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati ya mwaka 2024/2025
2) Kufatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa Mwaka 2024/2025.
3) Kufatilia utekelezaji wa Bajeti (kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo) kwa mwaka 2024/2025.
4) Kufatilia ukusanyaji wa mapato katika vitengo vya Serikali pamoja na kufanya ziara kwa Taasisi zake.

1:3 MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ilifanya kazi zake kama ifuatavyo: -

1) Pemba kuanzia tarehe 12/08/2024 hadi tarehe 16/08/2024,
2) Unguja kuanzia tarehe 19/08/2024 hadi tarehe 23/08/2024,
3) Pemba kuanzia tarehe 04/11/2024 hadi tarehe 08/11/2024,
4) Unguja kuanzia tarehe 11/11/2024 hadi tarehe 15/11/2024,
5) Pemba kuanzia tarehe 23/01/2025 hadi tarehe 25/01/2025,
6) Unguja kuanzia tarehe 27/01/2025 hadi tarehe 31/01/2025.

1.4 NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA

Katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa mujibu wa Kanuni, Kamati ilitumia njia na mbinu mbali mbali ikiwemo: -

1) Kufanya vikao na Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara husika kwa lengo la kupata taarifa juu ya mambo au maswala mahsusi ambayo Kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa watendaji wa taasisi hizo.

2) Kufanya ziara za ukaguzi katika miradi ya Maendeleo, sehemu za kazi na sehemu nyengine ambazo kwa namna moja ama nyengine zinahusika na utekelezaji wa majukumu ya Wizara husika.
3) Kufanya mikutano na Wafanyakazi pamoja na Wadau kwa lengo la kupokea maoni juu ya masuala mbali mbali ambayo Kamati ilikuwa inayafanyia kazi.

Kamati imebaini kwamba njia hizi ilizotumia zimeleta manufaa makubwa, kutokana na njia hizo kuwezesha kufahamu mafanikio na changamoto zinazoikabili Wizara na Idara na Taasisi husika katika utekelezaji wa majukumu yao.

1.5 HADIDU REJEA

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2024/2025 Kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo; -

a) Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.
b) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.
c) Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2024.
d) Hansard za Baraza za Mwaka 2024/2025.
e) Hotuba za Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii.

SEHEMU YA PILI – MAUDHUI

A: WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA UCHUKUZI

2.0 MUUNDO WA WIZARA.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi inaundwa na Idara tatu (3), Afisi kuu Pemba, Taasisi tisa (9) zinazojitegemea na Bodi mbili zinazosimamia sekta ya Ujenzi. Idara hizo ni; Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Mawasiliano na Afisi Kuu Pemba. Taasisi tisa (9) zinazojitegemea ni pamoja na; Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Mamlaka ya Usafiri Baharini, Shirika la Bandari Zanzibar, Shirika la Meli Zanzibar, Wakala wa Barabara Zanzibar, Wakala wa Serikali wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar, Shirika la Mawasiliano (ZICTIA) na Wakala wa Majengo Zanzibar. Bodi zinazosimamiwa na Wizara hii ni Bodi ya Usajili Wakandarasi na Bodi ya Usajili wa Wataalamu, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo.

2.1 PROGRAMU ZA WIZARA

Katika kutekeleza Majuku ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa wa mwaka 2024/2025, Wizara hii iliendelea na Programu zake Nne (4) kama zifuatavyo: -

a) Programu ya Usafirishaji:
b) Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)
c) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.
d) Programu ya Ujenzi na Majengo ya Serikali.

2.1. 1 PROGRAMU YA USAFIRISHAJI

Kamati ilichunguza utekelezaji wa Programu Kuu hii yenye lengo la kuimarisha Miundombinu na Huduma za Usafirishaji zilizobora, salama na endelevu. Programu hii inatekelezwa Taasisi zifuatazo: -

a) Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani.
b) Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar.
c) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
d) Wakala wa Barabara Zanzibar.
e) Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA)
f) Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)
g) Shirika la Meli Zanzibar
h) Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege

Katika ripoti hii Kamati inaelezea miongoni mwa utekelezaji wa Shughuli Kuu na Miradi inayotekelezwa na taasisi hizo hadi kufikia Mwezi Disemba 2024 kama ifuatavyo: -

2.1. 2 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI.

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani yenye jukumu la kusimamia watumiaji wa usafiri barabarani pamoja na utoaji wa huduma za usafiri barabarani pamoja na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya Usalama Barabarani, imefanikiwa kutekeleza yafuatayo; -

a) Kamati imebaini jumla ya vyombo vya moto 29,012 Unguja na Pemba vimekaguliwa sawa na asilimia 76 ya makadirio.
b) Mamlaka katika kipindi hiki imeweza kutoa jumla ya ruhusa za njia na usafirishaji 12,046 kwa gari zinazotoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo sawa na asilimia 108 ya makadirio.
c) Kamati ilipofuatilia suala la utoaji wa leseni za kujifundishia vyombo vya moto kwa madereva wanaojifundisha, ilibaini kuwa jumla ya leseni za madereva wanafunzi 13,237 zimetolewa Unguja na Pemba sawa na asilimia 109 ya makadirio.

2.1. 3 Mradi wa Kituo cha Ukaguzi wa Vyombo vya Moto:

Kamati ilipokea taarifa ya ujenzi wa kituo cha kisasa cha ukaguzi wa vyombo vya moto katika eneo ya Dole na iliarifiwa kwamba hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa jengo na miundombinu ya kurahisisha ufanisi wa shughuli inayokusudiwa kufanyika hapo ambapo Mradi huu umemalizika na kufunguliwa mwezi huu.

2.1. 4 Mradi wa Zims - Zanzibar Integrated Management System:

Kamati pia ilipokea taarifa za Mradi wa Zanzibar Intergrated Management Systerm ni mfumo mama wa Mamlaka unaotarajiwa kujumuisha moduli zote za utoaji wa huduma za usafiri na usalama barabarani Zanzibar. Kamati imebaini kwamba jumla ya moduli nane (8) zimekamilika katika mfumo huo na Mamlaka kwa sasa iko katika hatua za mwisho za kuwapa mafunzo wafanyakazi pamoja na wadau wengine wa sekta ya usafiri kwa ajili ya utekelezaji. Mradi huu unatarajiwa kuanza kazi mwezi huu wa Febuari 2025.

Changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani

a) Kuendelea kuwepo kwa Uhaba wa vyuo vya udereva hasa Vijijini.
b) Nidhamu ndogo na ukiukwaju wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Usalama Barabarani hasa kwa madereva hasa Boda boda.
c) Kuendelea kuwepo kwa tatizo kupakia kupita kiasi kwa gari zinazochukua wanafunzi (School Bus) sambamba na kupakia zaidi wa abiria mmoja katika Bobaboda.
d) Kuwepo na changamoto ya madereva wengi wa vyombo vya moto wakiwa na umri mdogo.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1. Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka na Wizara kwa ujumla kusimamia suala la uanzishwaji wa vyuo vya Udereva hadi vijini ikiwa ni njia moja wapo ya kuongeza uelea kwa wananchi juu ya masuala ya usalama wa barabarani.
2. Mamlaka kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika izidishe kasi ya Usimamizi wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Usalama barabarani na kuhakikisha inafuatwa hasa

kwa waendesha bodaboda na watumiaji wengine ili kupunguza ajali na vifo vinavyochangia kupunguza nguvu kazi ya Taifa.

3. Wizara iweke utararibu na miongozo maalum kwa vyombo vya Usafiri vinazochukua wanafunzi ili kupunguza tatizo la mrundikano na upakiaji mbaya wa wanafunzi katika vyombo hivyo.
4. Wizara na Serikali kwa ujumla ifikirie namna bora ya kudhibiti magari mazito kulingana na uwezo wa Barabara zetu ili ziendelee kudumu kwa muda mrefu ikiwa ni pamoja na kuzungumza mapema na Wakandarasi wanaokuja na magari makubwa wakati wa utekelezaji wa miradi yao.

2.1. 5 WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR.

Kamati pia ilifuatilia na kuchunguza utendaji wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar iliyopewa jukumu la Kusimamia matengenezo ya vyombo vya moto pamoja na kutoa ushauri wa ununuzi wa vyombo vya moto vya Serikali ili viwe katika ubora unaohitajika kisheria na kubaini kuwa Wakala imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Wakala kwa upande wa Unguja imefanikiwa kuzifanyia matengenezo jumla ya gari 735 za Serikali sawa na asilimia 98 ya makadirio ya gari 750. Aidha, imezifanyia matengenezo gari 53 za watu na mashirika binafsi sawa na asilimia 53 ya makadirio ya gari 100. Kwa upande wa Pemba, Wakala imefanikiwa kuzifanyia matengenezo jumla ya gari 130 za Serikali sawa na asilimia 25 ya makadirio ya gari 530.

(ii) Katika kuhakikisha taasisi za Serikali zinanunua magari na vyombo vyengine vyenye ubora unaoendana na wakati na matumizi ya taasisi husika, Wakala kwa upande wa Unguja imefanikiwa kutoa ushauri kwa taasisi 17 (14 ununuzi na 3 uuzaji) sawa na asilimia 106.2 ya makadirio.

(iii) Katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za Kiutawala na Kiufundi kwa wakati na kuhakikisha upatikanaji wa huduma hizo muda wote wa kazi, Wakala imefanikiwa kununuwa vitendea kazi, vipuri na vilainishaji.

Changamoto za Wakala wa Karakana Kuu ya Magari

Wakala wa Karakana Kuu ya Magari katika kutekeleza majukumu na shughuli zake, bado inaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo: -

a) Uhaba wa bajeti na fedha za matumizi ya kawaida.
b) Elimu ndogo kwa mafundi pamoja na uhaba wa mafundi katika vitengo husika na kukosekana kwa wataalamu wabobezi wa ufundi wa magari ya kisasa.
c) Uchakavu pamoja na kupitwa na wakati kwa miundombinu ya Karakana, mashine na vifaa kwa ajili ya huduma za kisasa za kiufundi.
d) Kuchelewa kulipa madeni kwa baadhi ya Taasisi za Serikali baada ya kupatiwa huduma na kupelekea Karakana kukusanya mapato madogo yasiyoridhisha.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.

1) Kamati inaendelea kuishauri Karakana kuomba kuruhusiwa kutumia mapato yatokanayo na matengenezo ya magari.
2) Wakala iweke utaratibu mpya wa malipo kwa wateja wote wanaopatiwa huduma ya matengenezo ambapo mteja atatakiwe kulipa kwanza kabla ya kufanyiwa matengenezo ya gari yake.

2.1. 6 IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI.

Kamati pia ilifuatilia utendaji kazi wa Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kusimamia na kuratibu miradi ya Maendeleo ya Wizara kama ifuatavyo: -

A) Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Mjini Unguja Kilomita 100.9: Hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi wa Disemba, 2024 jumla ya kilomita 84.25 kati ya kilomita 100.9 zinaendelea kujengwa na zipo katika hatua mbalimbali za usafishaji, tabaka la kifusi cha awali, tabaka la kifusi cha mwisho, lami na zege. Mradi huu umefikia asilimia 65 ya utekelezaji. Pia mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara za juu (Fly over) katika eneo la Amani lililofikia asilimia 65 na Mwanakwerekwe Round About ililofikia asilimia 90 kwa mujibu ya taarifa za Wizara.

B) Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Ndani zenye jumla ya Kilomita 275.9 Unguja na Pemba; Kamati pia ilifuatilia maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa Barabara za ndani Unguja na Pemba na kubaini kwamba kwa upande wa IRIS ASER JV, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Disemba,2024 utekelezaji wa jumla wa mradi huu umefikia asilimia 72.7**.** Jumla ya Kilomita 254.3 zimejengwa kwa hatua mbalimbali ikiwemo kilomita 98.91 za barabara zimekamilika kwa kiwango cha lami.

Kwa upande wa Kampuni ya MAWI ambayo imepewa jukumu la kuweka lami ya moto, utekelezaji wa jumla wa mradi huu umefikia asilimia 36.17. Hadi kufikia mwezi wa Disemba 2024, jumla ya Kilomita 77.82 zimewekwa lami Unguja na Pemba.

Changamoto katika Mradi wa Barabara za Ndani Unguja na Pemba

Pamoja na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mradi huu, Kamati imebaini changamoto mbalimbali zilizojitokeza na kusababisha kuathiri harakati za utekelezaji wake. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na; -

a) Kuchelewa kufanya Tathmini na kulipa Fidia;-
   - *(i)* Barabara ya Mfurumatonga-Mlilie Skuli nyumba moja (1)
   - *(ii)* Barabara ya Fukuchachani-Kidagoni Skuli-Kidoti nyumba na mazao.
   - *(iii)* Barabara ya Kajengwa-Koba-Kinandi-Mnarani nyumba 55
   - *(iv)* Barabara ya Jambiani Kibigija-Jambiani Mfumbwi
   - *(v)* Barabara ya Bwejuu-Viamboni-Kwa Lila
   - *(vi)* Barabara ya Mapofu-Tumbe-Kojifa-Bandarini nyumba 101
   - *(vii)* Barabara ya Micheweni-Kiuyu-Maziwa Ng'ombe nyumba 38
   - *(viii)* Barabara ya Mzambarau Takao-Mchangamdogo nyumba 4.
   - *(ix)* Barabara ya Ukutini-Mtangani Bandarini nyumba 16

b) Kukosekana kwa maeneo ya kupeleka maji yanayotolewa barabarani (**Discharge Point)** kwa baadhi ya barabara.

c) Kuchelewa kupata ruhusa na maamuzi katika maeneo ya kuchimba kifusi na mawe magumu (Mfano Kibuteni, Konde na Micheweni).

d) Kuchelewa kukabidhiwa Mkandarasi barabara za mbadala wa zilizopendekezwa kuondolewa.
e) Kuchelewa kuondolewa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo maji na umeme katika maeneo ya ujenzi.
f) Uwepo wa maeneo yanayohitajika kujengwa Madaraja makubwa ("Box Culvert") kutokana na kiwango cha maji yanayopita hususan kwa barabara kadhaa za Pemba ambapo kwa mujibu wa mkataba, mradi hautahusisha ujenzi wa madaraja makubwa.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.

1) Kamati inaishauri Wizara ana Serikali kwa ujumla kumalizia kufanya taratibu zote za fidia kwa wananchi waliobakia ambao wamepisha miradi ya mradi huu ili uweze Kwenda kwa haraka na kukamilika kwa muda uliopangwa.
2) Wizara iendelee kuhakikisha inakuwa na mashirikiano ya kisekta hasa maji na Umeme ili kuhakikikisha mkandarasi anafanya kazi zake bila ya wananchi kupata madhara makubwa wa wakati wa uhamishaji wa miundombini ya huduma za kijamii.
3) Wizara iangalie uwezekano wa kuingiza Madaraja makubwa ("Box Culvert") katika miradi kama hii kuondosha usumbufu na hasara inayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wake.
4) Wizara ya Ujenzi, Mawasiliani na Uchukuzi ishirikiane na Wizara ya Maji, Nishati na Madini ili kuhakikisha Bomba kubwa na kongwe linalosambaza maji katika Mji Mkongongwe haliathiriki kutokana na Ujenzi wa Barabara ya Kinazini- Bububu.

C) Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu za Zanzibar.

1) **Ujenzi wa Barabara ya Wete - Chake kilomita 22.1.** Ujenzi wa barabara hii unaendelea na hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Disemba, 2024 kazi zilizofanyika ni uwekaji wa kifusi kwa urefu wa kilomita 18.7 na uwekaji wa lami ngumu kwa eneo la kilomita 15 kuanzia meli tano hadi Mzambarau Takao.

Ukamilishaji wa kazi za ujenzi wa Madaraja 3 makubwa katika maeneo ya Piki, Machengwe na Weni. Kwa ujumla ujenzi wa Barabara hii umefikia asilimia 48.

2) **Ujenzi wa Barabara ya Tunguu - Makunduchi kilomita 48.5, Fumba – Kisauni kilomita 12, Chake – Mkoani kilomita 43.5.** Kamati pia ilihoji utekelezaji wa Mradi huu na Majibu ya Wizara ni kwamba hadi kufikia Mwishoni mwa Mwezi wa Disemba 2024 hakuna kazi iliyofanyika katika utekelezaji wa mradi huu. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Wizara tayari imekamilisha taratibu zote za Ujenzi wa barabara hizi.

3) **Ujenzi wa Barabara Kuu kilomita 277 Unguja na Pemba.** Kamati ilipohoji juu utekelezaji wa Mradi huu wenye lengo la kuzijenga barabara kuu za Unguja na Pemba zenye urefu wa km 277 kwa kiwango cha lami, iligundua kwamba kazi zilizofanyika ni ujenzi wa barabara ya Kizimbani – Kiboje km7.2, Barabara ya Uzi - Nga'ambwa na daraja lake km 8.7 na Kitogani – Paje km 13.1. Kwa ujumla ujenzi wa barabara hizi umeanza na unaendelea.

D) Mradi wa Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba: Kwa Upande wa mradi huu kazi zilizofanyika ni utambuzi na uwekaji wa alama za mipaka katika eneo linalokusudiwa kufanyiwa utanuzi wa Uwanja, Mapitio ya Michoro inayobainisha ukubwa wa eneo la Uwanja pamoja na majengo ya Utawala. Aidha Kamati imebaini kwamba kazi nyengine zilizofanyika ni kufanya Tafiti za udongo na maumbile ya ardhi pamoja na ulipaji wa fidia za Nyumba, Miti na Vipando kwa Wananchi wote wanaotarajiwa kupisha utanuzi huo.

E) Mradi wa Ujenzi wa Bandari Shirikishi ya Mangapwani. Kwa upande wa Ujenzi wa Bandari ya Makontena Mangapwani, Kamati imebaini kwamba Wizara inaendelea na matayarisho kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo kupitia Kampuni ya CHEC ambayo inafanya kazi hiyo. Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa Barabara za ndani (ring road) katika eneo la mradi wa Bandari Jumuishi ya Mangapawani zenye urefu wa kilomita 12. Hadi kufikia

mwishoni mwa mwezi Disemba 2024, jumla ya kilomita 5.8 tayari zimeshawekwa lami ngumu. Ujenzi wa barabara hii umefikia asilimia 43 ya utekelezaji.

2.1. 7 WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR.

Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa na Wakala wa Barabara ni Ujenzi wa Barabara ya Abrahman Al Sumait km 0.8 kwa kiwango cha lami, Ujenzi wa Barabara ya Mchangani (Dunga) - Msikitini km 1.1km kwa kiwango cha lami, Ujenzi wa barabara za ndani za Kizimkazi zenye jumla ya urefu wa kilomita 6.59 kwa kiwango cha lami, Ujenzi wa Barabara ya Mgelema- Wambaa km 4.2 kwa Kiwango cha Lami; Ujenzi wa barabara za ndani kwa kiwango cha kifusi kwa hatua ya kwanza kilomita 3 kwa kiwango cha kifusi, Matengenezo ya dharura (Emergence work) Unguja na Pemba; na Matengenezo ya Kawaida ya Barabara (Routine patchwork);

Changamoto za Wakala wa Barabara

a) **Uchache wa Vifaa vya Ujenzi wa Barabara:** Wakala bado inakabiliwa na tatizo la uhaba wa vifaa vya ujenzi ukilinganisha na kazi zilizopo Unguja na Pemba. Kamati ibebaini kuwa hali hii, inapelekea Wakala kushindwa kutimiza majukumu yake kama inavyotakiwa.

b) **Uvamizi wa Maeneo ya Hifadhi ya Barabara kwa Ujenzi Holela:** Kamati imebaini kuwa bado changamoto hii inatokana na usimamizi mdogo wa sheria zilizopo kwa taasisi mbali mbali zinazohusika na masuala ya ujenzi.

c) **Wizi na Uharibifu wa Alama za Barabarani:** Kamati inaendelea kuripoti Changamoto hii ya muda mrefu ambayo inaendelea kujitokeza kutokana na madai ya ugumu wa usimamizi wa suala hili na kutokuwepo mashirikiano baina ya Serikali za Mitaa na vyombo vya Ulinzi na Usalama katika kuchukua hatua kwa wanaobainika kufanya kosa hili.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.

1) Bado Kamati inaendelea kuishauri Wizara kufanya mazungumzo na taasisi mbali mbali ili kuweza kusaidiana katika kusimamia utekelezaji wa sheria zilizopo na kuweza kudhibiti changamoto ya uvamizi wa hifadhi ya barabara kwa shughuli za ujenzi na biashara.
2) Wizara iendelee kuchukua hatua za kutoa taaluma kwa jamii juu ya umuhimu wa uwepo na matumizi ya alama za barabarani.

2.1. 8 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)

Mamlaka ya Usafiri Baharini imepewa jukumu la usimamizi na udhibiti wa ulinzi na usalama wa meli na bandari, Usajili wa meli, Utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo vya baharini, Ukaguzi wa meli na vyombo vidogo vidogo, usimamizi wa mazingira ya bahari yatokanayo na shughuli za meli pamoja na Uchunguzi wa ajali za baharini. Hadi Disemba 2024, Mamlaka ya Usafiri Baharini imetekeleza majukumu yao vizuri ikiwemo: -

(i) Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2024, Mamlaka ilipanga kusajili Meli **7** za ndani hadi kufikia mwezi wa Disemba 2024, ilisajili meli **8** za ndani sawa na asilimia **114** ya makadirio. Kwa upande wa Meli za kimataifa ilisajili Meli **207** za nje **sawa** na asilimia **172** ya makadirio.

(ii) Mamlaka ilipanga kusajili jumla ya vyombo Vidogo Vidogo **675** ambapo hadi kufikia Disemba, 2024, ilisajili vyombo vidogo vidogo **1058** sawa na asilimia **156** ya makadirio. Pia Mamlaka imefanikiwa kutoa leseni **850** za Manahodha waliofaulu mitihani na kupewa vyeti vya unahodha.

(iii) Hadi kufikia Disemba, 2024 jumla ya mabaharia **763** wamethibitishwa (endorsement) vyeti vyao vya umahiri (certificate of competency) sawa na asilimia **146** ya makadirio.

(iv) Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024, Mamlaka ilikadiria jumla ya abiria **1,244,453** kusafiri katika bandari za Unguja na Pemba. Hadi kufikia Disemba, 2024, idadi halisi ya abiria waliosafiri walikuwa ni **1,069,928** ambayo ni sawa na asilimia **85** ya makadirio.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.

1) Kamati inaishauri Wizara kupitia Mamlaka ya Usimaizi wa Usafiri wa Baharini kuwashajihisha wawekezaji zaidi katika sekta ya Usafiri wa Baharini ili kusaidiana na serikali katika kupunguza kero ya usafiri wa majini kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

2) Kamati inaendelea kusisitiza kwa Mamlaka usimamizi ya idadai ya abiria na mizigo katika vyombo vya usafiri wa majini ili kuhakikisha huduma hii inakua salama na bila ya kusababisha madhara kwa abiria na mizigo.

2.1. 9 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC)

Kamati pia ilifuatilia utendaji wa Shirika la Bandari ambapo imebaini kuwa Shirika hilo limepata mafanikio katika juhudi zake za kuboresha huduma na kuongeza ufanisi. Baadhi ya mafanikio hayo ni: -

(i) Kuwa na bandari kavu ya kisasa katika eneo la Maruhubi kupitia uwekezaji wa Kampuni ya Zanzibar Multipurpose Terminal (ZMT).

(ii) Kuanza kutumika bandari ya Mkoani katika kupokea meli za makontena.

(iii) Kukabidhi bandari ya Mkoani kwa muwekezaji ambae ni Kampuni ya Bandari ya Fumba.

(iv) Shirika la Bandari limefanikiwa kuboresha miundombinu yake, ikiwemo upanuzi wa gati, kuongeza maghala ya kuhifadhi mizigo na ununuzi wa vitendea kazi.

(v) Kutumia teknolojia ya kisasa kupitia mifumo ya usimamizi wa mizigo na vifaa vya kisasa vya upakiaji na upakuaji wa mizigo.

(vi) Ushirikiano na sekta binafsi katika uendeshaji wa baadhi ya huduma za bandari umeongeza ufanisi na ubunifu katika utoaji wa huduma.

(vii) Imeweza kuandaa Mpango wa Maboresho wa utoaji wa huduma za bandari.

UJENZI WA BANDARI YA SHUMBA

Kamati ilijiwekea ratiba za kukaguwa mradi wa Kimkakati wa Ujezi wa Bandari ya Shumba kila wakati ilipofanya shughuli zake huko Pemba. Hadi mara ya mwisho ilipokagua Mradi huo Januari 23, 2025 kwa mujibu wa Maelezo ya Wizara, Mradi huo umefikia asilimia 72.5%. Aidha, Kamati imeshuhudia harakati za kuanza kujengwa ukuta wa eneo lote la Bandari hiyo ambalo litaenda sambamba na ujenzi wa Banda la Abiria.

Changamoto za Shirika la Bandari

Shirika la Bandari limekabiliwa na changamoto kadhaa licha ya mafanikio hayo, changamoto hizo ni pamoja na ;-

a) Kuvamiwa kwa maeneo ya minara.
b) Msongomano wa abiria, bodaboda na gari nje ya mlango mkuu bandarini, suala ambalo linatoa sura mbaya na kupunguza haiba ya Mji wa Zanzibar pamoja na kuleta kero kwa watumiaji wengine wa barabara na kuisalama.
c) Ukumbi wa watu mashuhuri (VIP) kutumiwa kwa pamoja na abiria wenye tiketi za Daraja la Kwanza.
d) Kukosekana na kuchelewa kwa vifaa vya utendaji wa kazi kwenye eneo la Mradi wa Bandari ya Shumba kunakosababisha kuchelewa kwa kazi na kupoteza muda.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.

1) Kamati inalishauri Shirika la Bandari kutafuta hati miliki maeneo yake yote pamoja na kuyahami kwa kuyawekea uzio sambamba na kuweka walinzi waaminifu ili kuepusha uvamivi kwa shughuli za kilimo na makaazi katika maeneo hayo.

2) Shirika la Bandari kwa kushirikiana na taasisi nyengine ikiwemo Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa Mjini pamoja na Vikosi vyengine lihakikishe linaweka mikakati Madhubuti ya kulifanyia kazi suala la msongomano wa abiria, gari na bodaboda Bandarini.

3) Kamati bado inaendelea kusisitiza kuwekwa utaratibu maalum utakaozingatia matumizi sahihi ya eneo la watu mashuhuri (VIP) katika Bandari ya Zanzibar na Mkoani.

4) Kamati inamtaka Mkandarasi wa Bandari ya Shumba (**Kampuni ya Comfix & Engineering Smart Solution)** kuwa na mashirikiano mazuri kwa viongozi wanaokwenda kukaguwa mradi huo ili waweze kusikia mafanikio na changamoto zinazomkabili kutoka kwake moja kwa moja badala ya kuwakwepa.

2.1. 10 SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati pia ilifuatilia taarifa za Shirika la Meli Zanzibar ambalo miongoni mwa majukumu yake ni kutoa huduma za uendeshaji wa meli ndani na nje ya nchi pamoja na kutoa huduma za uwakala kwa meli zinazoingia katika bahari ya Zanzibar.

Maendeleo ya Matengenezo ya Meli ya MV Mapinduzi II

Katika taasisi hii, Kamati ilishawishika zaidi na taarifa za Meli ya MV Mapinduzi II ambapo tumebaini kwamba hadi kufikia Mwezi Disemba 2024 Matengenezo yake yameshafikia asilimia 90, huku meli ikisubiri kwenda chelezoni Mombasa nchini Kenya kukamilisha matengenezo hayo. Hata hivyo Kamati iliarifiwa kwamba mnamo wiki ya pili ya mwezi wa Febuari, 2025, Meli ya MV Mapinduzi II, ilitarajiwa kufanyiwa majaribio makubwa kwa kuipeleka Pemba na kurudi. Majaribio haya yakikamilika kwa mafanikio, meli itapelekwa chelezoni Mombasa Nchini Kenya kwa ajili ya kuangaliwa kwa kina sehemu ya chini ya meli hiyo.

Ununuzi wa Boti za Mwendo wa Kasi za Serikali

Kamati pia ilifanya utafiti wa kujua hatua ya Serikali za kutafuta boti zake za mwendo wa kasi ili kurahisisha huduma za Usafiri wa majini kati ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam. Kamati imebaini kuwa tarehe 17 Julai, 2024, Shirika liliingia makubaliano ya ujenzi wa boti hizo na Kampuni ya Synergy Shipbuilder ya India, ambapo malipo ya awali ya USD 2.5 milioni yameshalipwa kwa Mjenzi. Aidha, Ujenzi unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi wa Febuari, 2025. Mchoro wa boti hizo utawasilishwa katika Shirika mnamo mwezi

wa Febuari, 2025 baada ya kuthibitishwa na 'Classification society (RINA) ambapo Mkandarasi anaendelea kukusanya vifaa kwa ajili ya ujenzi wa boti hizo.

Changamoto za Shirika la Meli Zanzibar

Kamati imebaini kuwa katika kuendesha shughuli zake, bado Shirika linaendelea kukabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo; -

a) Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma katika shughuli za kibiashara za Shirika.

b) Kutokuwepo na mfumo wa mishahara ya ubaharia na kutotambulika katika taasisi za kiutumishi za Serikali.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Kamati bado inaisisitiza Wizara na Serikali kwa ujumla kuangalia uwezekano wa kuliruhusu Shirika kununua vifaa au vipuri moja kwa moja kutoka kwa wasambazaji hata kama mara nyingi wasambazaji hao huwa kutoka nje ya nchi ambao hawamo katika mfumo wa manunuzi Serikalini.

2) Kamati inaomba Serikali kupitia Wizara ya Utumishi kuangalia uwezekano wa kuweka mfumo wa mishahara ya mabaharia kama inavyohitajika kulingana na kada hiyo.

2.1. 11 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, nayo ni miongoni taasisi inayounda Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na kutekeleza Programu ya Usafirishaji kwa kuviendesha, kuvisimamia, na kuviendeleza viwanja vya ndege vya Serikali pamoja na kusimamia usalama kwa safari za abiria na mizigo katika viwanja hivyo. Kamati imebaini kwamba katika kipindi hiki cha Ufuatiliaji Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Kuongezeka kwa abiria waliohudumiwa kwa asilimia 11.4 kutoka abiria 1,180,436 kwa kipindi cha robo mbili mwaka wa fedha 2023/24 hadi kufikia abiria 1,290,284 kwa robo mbili mwaka wa fedha 2024/25

(ii) Kuongezeka idadi ya mzigo kwa asilimia 16 kutoka tani 1999.97 kipindi cha robo mbili mwaka wa fedha 2023/24 hadi kufikia tani 2,328 kwa robo mbili mwaka wa fedha 2024/25.

(iii) Kuongezeka kwa mapato ya Mamlaka kwa asilmia 53 kutoka shilingi Bilioni 18,818,330,676.88 kwa robo mbili mwaka wa fedha 2023/24 hadi kufikia shilingi Bilioni 23,501,027,432.67 kwa robo mbili mwaka wa fedha 2024/25.

(iv) Kupokelewa kwa mashirika mapya Manne (4) ya ndege ambayo ni Jambo Jet, fly One, Tui na Bulgaria.

(v) Kuweka taa mpya 136 za kuongezea ndege (AGL lights) katika uwanja wa AAKIA.

2.2. 1 PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

Kamati pia ilifuatilia utekelezaji wa Programu hii inayotekelezwa na Idara ya Mawasiliano na Shirika la Mawasiliano Zanzibar ambyo lengo lake kuu ni kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za TEHAMA zilizo salama na endelevu Unguja na Pemba. Katika kipindi hiki cha tathmini ya ufuatiliaji wa Utekelezaji kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo: -

2.2. 2 IDARA YA MAWASILIANO

Idara ya Mawasiliano imeendelea na program ya kutoa mafunzo ya kidijitali kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii ambapo jumla ya wananchi 1190 wamepata mafunzo pamoja na huduma mbalimbali zinazotolewa katika vituo hivyo. Mafunzo hayo yanajumuisha program ya mafunzo ya usalama wa mtandao. Aidha, katika kipindi hicho zoezi la uhakiki wa Anuani za Makaazi liliendelea ambapo jumla ya anuani za makaazi 33,358 zimehakikiwa na jumla ya nyumba na majengo 4,828 zimewekewa anuani za makaazi.

Vilevile, Kamati imebaini kwamba Idara inaendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo yote ya Zanzibar, ambapo katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2024 ruhusa za ujenzi wa minara katika maeneo 12 zimetolewa.

2.2. 3 SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR (ZICTIA)

Kamati ilipofuatilia utekelezaji wa Shirika la Mawasiliano (ZICTI) imebaini kuwa pamoja na shughuli za kawaida, Shirika lina miradi ya Maendeleo Mitatu na michakato ya utekelezaji katika kipindi hiki cha upimaji ni kama ifuatavyo: -

(i) **Mradi wa Kuimarisha njia ya kusafirishia Mawasiliano kutoka Unguja Hadi Pemba kupitia Minara.**

Katika mradi huu ZICTIA inaendelea na taratibu za manunuzi ili kumpata Mkandarasi wa kufanya kazi hiyo ikiwa na lengo la Kufanya maboresho ya Mawasiliano (Microwave Transmission System) kwa minara inayoounganisha mawasiliano baina ya Unguja (Nungwi) na Pemba (Kichunjuu).

(ii) **Mradi wa Kutayarisha Mpango Mkuu (Master Plan) wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar.** ZICTIA imeendelea na mchakato wa kuhakikisha inatekeleza Mradi huu ambapo kwa sasa ZICTIA tayari imepata ufadhili kutoka African Development Bank (AFDB) kwa lengo la kufanya upembuzi yakinifu wa Utengenezaji wa Mpango Mkuu wa Mji wa Kidijitali Zanzibar (Zanzibar Cyber City Master Plan) – Fumba

(iii) **Mradi wa Kuhamisha na kurejesha Mkonga unaoathirika na Ujenzi wa Barabara mbali mbali Zanzibar**. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2024, kazi ya kuhamisha Mkonga kutokana na matengenezo ya barabara imeendelea na kufikia Kilomita za barabara zisizopungua 250 katika njia (route) mbali mbali. Aidha, ZICTIA imefanikiwa kufanya na kukamilisha matengenezo hayo katika maeneo ya Mndo Kizimbani, Chukwani, Uwanja wa Ndege, Mazizini na Tunguu hadi Makunduchi.

2.3.3 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA UCHUKUZI.

Katika kufuatilia utekelazji wa Programu hii inayotekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango Sera na Utafiti na Afisi Kuu Pemba Kamati imebaini kwamba kumekuwa na mafanikio makubwa ikiwemo: -

(i) Kukamilisha Sera ya Mageuzi ya Kidijtali ambayo ipo katika hatua za kuwasilishwa katika kikao cha Makatibu Wakuu.

(ii) Kuzifanyia mapitio sheria tatu ambazo ni Sheria ya Wakala wa Barabara, Sheria ya Mamlaka ya Usafiri Barabarani pamoja na Tangazo la Kisheria la Uanzishwaji wa Wakala wa Majengo.

(iii) Kuratibu na kusimamia malipo ya fidia za wananchi pamoja na kushugulikia malalamiko ya Wananchi kwa maeneo mbali mbali yanayoendelea na ujenzi wa miundo mbinu ya barabara Unguja na Pemba.

MAENDELEO YA TATHMINI NA FIDIA ZA WANANCHI WALIOPISHA MIRADI HADI TAREHE 31 DISEMBA 2024.

Kamati ilitaka kutambua maendeleo ya Tathmini na Fidia kwa wananchi waliopisha miradi mbai mbali inayotekelezwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Unguja na Pemba hadi kufikia Disemba 2024 na kwa mujibu wa vielelezo vya Wizara hii kwa upande wa Unguja ni kama kama ifuatavyo:-

Jadweli nambari 1. Malipo ya Fidia na Madeni kwa Wananchi katika Mradi wa Barabara za Mjini. (Chanzo WUMU, Disemba 2024)

Na	**Barabara**	**Tathmini**	**waliolipwa Fidia**	**Madeni ya Fidia**	**Wanao dai Fidia.**
1	Barabara ya Chukwani – Buyu Kilomita 3.5	1	43	0	0
2	Barabara ya Mwanakwerekwe GAPCO – Kwerekwe Skuli – Kanisani – KwaMchina and Associated Road kilomita 5.99	1	29	0	0
3	Barabara ya Msumbiji Kinyang'unya – Mwanakwerekwe and Associated kilomita 5.43	1	15	93,862,000	3
4	Fidia kwa maeneo ya Ujenzi wa Fly over ya Mwanakwerekwe	1	12	164,358,000.00	1
5	Fidia kwa maeneo ya Ujenzi wa Fly over ya Amani	2	16	11,306,206,525.00	117

***Jadweli* nambari 2**. *Malipo ya Fidia na Madeni kwa Wananchi katika Mradi wa Barabara za Ndani – Unguja. (Chanzo WUMU, Disemba 2024)*

Na	Barabara	Tathmini	waliolipwa Fidia	Madeni ya Fidia	Wanaodai Fidia.
1	Barabara ya Tunguu- Ndijani Mseweni – Mkwajungoma kilomita 7.8	1	1	13,800,000.00	1
2	Barabara ya Fuoni Kibondeni – Jumbi Sokoni	1	1	0	0
3	Barabara ya Mwera Polisi Fuoni Kibonde Mzungu kilomita 6.1	1	1	0	0
4.	Barabara ya Dunga - Zuze	1	22	0	0
5.	Barabara ya Kajengwa -Koba-Kinandi Mnarani	1	0	1,721,180,000	116
6.	Barabara ya Fukuchani-kidagoni skuli -Kidoti	2	0	140,485,000	109

Jadweli nambari 3**. Malipo ya Fidia na Madeni kwa Wananchi katika Ujenzi wa barabra ya Jozani – Charawe – Ukongoroni, Fuoni – Tunguu* ***(*Chanzo WUMU, Disemba 2024)*

Nam	Barabara	Tathmini	waliolipwa Fidia	Madeni ya Fidia	Wanaodai Fidia.
1	Fuoni – Tunguu	1	1	0	0
2	Jozani – Charawe – Ukongoroni	2	31	172,990,000.00	42

Jadweli namba 4: UfMalipo ya fidia katika Mradi wa Ujenzi wa Bandari jumuishi ya Mangapwani.

Nam	**Barabara**	**Tathmini**	**waliolipwa Fidia**	**Madeni ya Fidia**	**Wanaodai Fidia.**
1.	Barabara ya Ringi Road	4	546.	1,055,092,000	417
2.	Ujenzi wa Nyumba za Fidia	1	346	731,535,000	54

Kiambatanisho nambari 5*. Malipo ya fidia na tathmini iliyofanyika katika Uimarishaji wa miundombinu ya Mawasiliano Fumba. (Chanzo WUMU, Disemba 2024)*

Nam	**Idadi ya Tathmini**	**Waliolipwa Fidia**	**Madeni ya Fidia**	**Wanaodai Fidia.**
1.	2	396	6,869,437.50	5

Jadweli nambari 6 *: Barabara ya Chake – Wete (Chanzo WUMU, Disemba 2024)*

TAREHE	**FEDHA ZILIZOINGIZWA KWA AJILI YA MALIPO YA FIDIA**	**IDADI YA WALIPWA FIDIA**	**ZILIZOLIPWA**	**BAKAA**
Septemba,2022	1,767,896,736	561	8,876,989,951	66,029,769
Februari,2023	5,893,507,189			
Machi, 2023	1,000,000,000			
May, 2023	281,615,795			
JUMLA	**8,943,019,720**	**561**		

Jadweli nambari 7: *Madeni ya fidia hadi 31/12/2024 kupitia ripoti mbali mbali za Mthamini Mkuu wa Serikali (Chanzo WUMU, Disemba 2024)*

AINA YA RIPOTI	**IDADI YA WALIPWA FIDIA**	**KIWANGO CHA FEDHA**
Ripoti ya vipando/miti	1,114	564,875,800
Ripoti za majengo kuondosha vikwazo vya ujenzi	51	680,760,000
	13	114,325,000
Ripoti ilijumuisha maeneo mbali mbali ya miradi ya wizara	32	127,863,000
Ripoti ya kuondosha vikwazo	1 (Msikiti Mz/Takao)	74,704,250
JUMLA YA DENI	**-**	**1,562,528,050**

Jadweli nambari 8: Barabara Za Ndani – Pemba *(Chanzo WUMU, Disemba 2024)*

MADENI YA FIDIA KWA BARABARA MBALI MBALI ZA NDANI		
JINA LA BARABARA/ENEO	**WALIPWA FIDIA**	**DENI**
Barabara ya Wingwi Mapofu – Tumbe Bandarini 1	37	776,250,000
Chanjaani – Pujini 5km	6	112,503,000
Ukutini – Mtangani Bandarini 4.6km Pujini	22	182,200,000
Kipapo – Mgelema – Wambaa 9.3km	1	10,460,000
Vitongoji Borrowpit	15	53,177,000
JUMLA		**1,134,590,000**

Jadweli nambari 9: *Malipo ya Fidia Kwa Mradi Wa Utanuzi wa Uwanja wa Ndege Pemba (Chanzo WUMU, Disemba 2024)*

TAREHE	**FEDHA ZILIZOINGIZWA KWA AJILI YA MALIPO YA FIDIA**	**IDADI YA WALIPWA FIDIA**	**ZILIZOLIPWA**	**BAKAA**
Novemba, 2023	12,627,519,000	789	12,877,342,736 (Kwa watu 946)	2,276,700,994
Ogasti	2,526,524,730	215		
JUMLA	**15,154,043,730**	**1,004**		

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.

1) Kamati inaendelea kuwasisitiza watendaji wa Wizara kuendelea kuwa waadilifu katika suala zima la Fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya Wizara ili kuepusha malalamiko yasiyokuwa ya lazima ya wananchi kwa Serikali yao.

2.4. 1 PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO YA SERIKALI.

Programu hii inasimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA), Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo (AEQSRB) na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (ZCRB). Utekelezaji wa programu kwa taasisi zinazosimamia ni kama ifuatavyo: -

2. 4.2 WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR

Wakala wa Majengo Zanzibar iliyopewa jukumu la kusimamia majengo ya Serikali pamoja na kutoa huduma ya Ushauri Elekezi kwa miradi mbalimbali ya Serikali katika kipindi hiki cha ufuatiliaji imefanikiwa; -

(i) Kutayarisha nyaraka za ujenzi (ramani, BoQ) 11 ambazo ni sawa na asilimia 68.75 ya makadirio.

(ii) Imesimamia miradi ya ujenzi **36** sawa na asilimia **116.13** ya makadirio.

(iii) Imeratibu vikao vya Wadau vya kupitia na kutoa maoni kuhusu rasimu ya sheria ya Wakala wa Majengo na kwa sasa imewasilishwa Wizarani.

2. 4.3 BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI

Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha upimaji wa utekelezaji, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imefanikiwa kusajili wakandarasi 27 pamoja na kusajili miradi 174 Unguja na Pemba. Aidha, Jumla ya miradi 376 ilikaguliwa, miradi 266 ilionekana kuwa na upungufu hivyo wakandarasi au wamiliki wa miradi hiyo waliitwa katika ofisi za bodi na kupewa maelekezo.

2.2.24 BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO ZANZIBAR.

Hadi kufikia Mwezi Disemba, 2024, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriji Majengo imefanikiwa kuteleleza yafuatayo: -

(i) Bodi ilikadiria kusajili jumla ya wataalamu 55 na Kampuni za ushauri 10, ambapo ilifanikiwa kusajili jumla ya wataalamu 51 na Kampuni za ushauri 15 katika fani za usanifu, uhandisi na ukadiriaji ujenzi.

(ii) Bodi ilikadiria kusajili miradi 151 na imefanikiwa kusajili jumla ya miradi 173 kwa upande wa Unguja na miradi 16 kwa upande wa Pemba. Miradi hiyo inajumuisha Ujenzi wa Majengo ya Biashara, Nyumba za Makaazi, Hoteli, Skuli, Nyumba za ibada, Ofisi na mengineyo.

(iii) Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024 Bodi ilikadiria kukagua jumla ya miradi 95 ya ujenzi wa majengo na imefanikiwa kufanya ukaguzi katika miradi ya U91 ya ujenzi katika maeneo mbali mbali ya ujenzi Unguja na Pemba.

B: WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

3:0 UTANGULIZI

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar imepewa majukumu ya kusimamia na kuendeleza Sekta za Ardhi na Makaazi kupitia Taasisi zake.

3:1 MUUNDO WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

Kimuundo Wizara hii inajumuisha Sekta tatu ambazo ni Mipango na Uendeshaji, Ardhi pamoja na Makaazi ambapo Sekta hizi ni za utoaji wa huduma kwa jamii. Kiutendaji Sekta hizi zimegawika katika Taasisi saba na Bodi Tendaji mbili kama ifuatavyo: -

	SEKTA YA MIPANGO NA UENDESHAJI	
1.	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	Inaongozwa na Mkurugenzi
2.	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	Inaongozwa na Mkurugenzi
3.	Ofisi ya Mdhamini Pemba	Inaongozwa na Afisa Mdhamini
	SEKTA YA ARDHI	
4.	Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali	Inaongozwa na Mthamini Mkuu wa Serikali
5.	Mahkama ya Ardhi	Inaongozwa na Mwenyekiti
6.	Kamisheni ya Ardhi (CoLA)	Inaongozwa na Katibu Mtendaji
	SEKTA YA MAKAAZI	
7.	Shirika la Nyumba	Linaongozwa na Mkurugenzi Mkuu
8.	Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba	Inaongozwa na Mwenyekiti
9.	Divisheni ya Kondominio	Inaongozwa na Mwenyekiti
10	Idara ya Maendeleo ya Makaazi	Inaongozwa na Mkurugenzi

3.2 SEKTA YA ARDHI

Sekta hii inaundwa na Kamisheni ya Ardhi, Mahakama ya Ardhi na Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ambapo ina jukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi na umiliki (Secure of land Tenure) kwa wananchi.

3:2:1 KAMISHENI YA ARDHI

Kamati ilipofuatilia utendaji wa Kamisheni ya Ardhi imebaini kwamba hadi kufikia Disemba 2024, Kamisheni imefanikiwa kutekeleza majukumu yake katika nyanja tofauti, ambapo miongoni mwa mafanikio yake ni kama ifuatavyo: -

(i) Jumla ya hati za haki ya matumizi ya Ardhi 295 zimeandaliwa pamoja na kutayarisha Mikataba 199 ya ukodishaji wa Ardhi Unguja na Pemba

(ii) Imefanikiwa kutoa hati za EKA TATU 406 pamoja na kufanya ukaguzi wa maeneo 65 ya EKA TATU.

(iii) Imefanya ukaguzi wa maeneo 117 ya uhaulishaji kwa Unguja na maeneo 64 kwa upande wa Pemba.

(iv) Imepima maeneo 455 ya viwanja kutokana na maombi ya wananchi ambapo 316 kwa upande wa Unguja na 139 kwa Pemba.

(v) Imetayarisha mpango wa kina wa Ardhi ya Akiba kwa eneo la Kizimkazi na Kibuteni kwa upande wa Unguja na eneo la Mvumoni – Chakechake na Kojani kwa Pemba.

(vi) Imeendelea na zoezi la uwekaji wa mabango katika maeneo ya Mwera Pongwe, Mwakaje, Matemwe na Nungwi kwa ajili ya kuzuia uvamizi pamoja na kudhibiti ujenzi holela katika maeneo ya Ardhi ya Akiba.

(vii) Imeanda miongozo 1,430 ya ujenzi ambapo miongozo 1,231 kwa Unguja na 199 kwa Pemba.

3:2:2 UJENZI WA SEHEMU YA UZIO NA TANGI LA MAJI KATIKA MASJALA YA ARDHI MWANAKWEREKWE

Katika kipindi hiki cha ufuatiliaji Kamati ilitembelea vitengo mbali mbali vya Kamisheni ya ikiwemo Masjala ya Ardhi ya Wilaya ya Magharibi B Mwanakwerekwe. Utafiti uliofanywa na Kamati umebaini kwamba Kamisheni baada ya kujitokeza uhitaji wa utoaji wa huduma ya Utambuzi kwa Wananchi, Serikali imeona ipo haja ya kujenga vituo vya Usajili wa Ardhi kwa kila Wilaya ambapo kwa hatua za awali vituo vya masjala vimejengwa Wilaya ya Maghrib 'B' eneo la Mwanakwerekwe na Wilaya ya Kusini Unguja eneo la Makunduchi.

Hata Hivyo, Kamati ilipotembelea Masjala ya Mwanakwerekwe iliarifiwa kwamba Kamisheni imetumia jumla ya **TZS 56,148,175.00/-** kwa ajili ya shughuli ujenzi wa ukuta na mnara wa maji unaojengwa na Mkandarasi KYRENIA ENGINEERING COMPANY LTD.

Changamoto za Kamisheni ya Ardhi

Katika nyakati tofauti za mizunguko ya kazi za Kamati tulikutana na watendaji wa Kamisheni ya Ardhi na katika mahojiano yetu, Kamati ilibaini kwamba bado Kamisheni inaendelea na changamoto zilizoibuliwa katika ripoti zilizopita ambazo miongoni mwao ni:-

a) Kuendelea na uhaba na uchakavu wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya kusimamia utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli zilizopangwa.
b) Kiwango kidogo cha uelewa wa jamii juu ya dhana ya utawala na usimamizi wa Ardhi.
c) Uvamizi wa maeneo kwa matumizi tofauti na yale yaliyoainishwa katika mipango mikuu ya matumizi ya ardhi kama vile maeneo ya miundombinu, kilimo na hifadhi za misitu.
d) Ukosefu mkubwa wa Mipango Miji na Vijiji, suala ambalo linapelekea ujenzi holela na kusababisha changamoto nyengine ya ugumu wa kupeleka huduma za kijamii ikiwemo barabara, mifumo ya maji safi na maji machafu na zimamoto.

MAAGIZO, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuharakisha taratibu zilizobaki ili kukamilisha mradi wa Utambuzi na Usimamizi wa Ardhi (LARIS) ili kupunguza Migogoro ya Ardhi inayoendelea katika jamii.
2) Kamati inaendelea kuishauri Kamisheni na Wizara kwa ujumla kufuatilia Serikalini kupitia Tume ya Utumishi wa Umma suala la upatikanaji wa vibali vyengine vya ajira ili waweze kutekeleza majukumu kwa ufanisi zaidi.
3) Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuwaangalia wafanyakazi wanaohusika na masuala ya utambuzi na upimaji wa Ardhi kwa jicho la huruma kutokana na mazingira magumu na hatarishi wanayofanyia kazi.
4) Kamati inaishauri Kamisheni ya Ardhi kuzitumia Taasisi za Serikali kwa ajili ya kupata Ushauri wa Kitaalamu kuhusu ujenzi wa miradi yao, kwani kuzitumia Kampuni binafsi mara nyingi wao huangalia faida kubwa zaidi ya uzalendo.
5) Kamati inashauri kwamba utaratibu ulioanzishwa wa uwekaji wa Miji Mipya uende sambamba na ushirikishwaji wa Taasisi zote zinazohusika na uwekaji wa miundombinu ili huduma za kijamii zifikishwe mapema na kwa uharaka katika maeneo husika kwa ajili ya kuepusha usumbufu wa kimiundombinu na kimazingira unaoweza kutokea hapo baadae.

3:2:3 MAHKAMA YA ARDHI.

Katika kipindi hiki Mahkama ya Ardhi Zanzibar imeendelea na jukumu lake la msingi la kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri ya migogoro ya Ardhi yaliyowasilishwa na wananchi pamoja na Taasisi mbalimbali. Hadi kufikia Disemba 2024, Mahkama ya Ardhi imepokea jumla ya kesi mpya **128** ambazo zimefunguliwa Unguja na Pemba. Aidha, Mahkama imeendelea kusikiliza kesi hizo pamoja na za awali ambapo kesi Tisiini **(90)** zimetolewa maamuzi, sawa na wastani wa **asilimia 57** kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2024, kama mchanganuo ufuatao unavyoonesha hapo chini: -

SN	MKOA HUSIKA	KESI MPYA ZILIZOPOKELEWA	KESI ZILIZOTOLEWA MAAMUZI	KESI ZINAZOENDELEA MAHAKAMANI
1	MJINI MAGHARIBI	42	34	94
2	KASKAZINI UNGUJA	21	13	33
3	KUSINI UNGUJA	24	10	53
4	KASKAZINI PEMBA	14	08	23
5	KUSINI PEMBA	27	25	41
	JUMLA KUU	**128**	**90**	**244**

Changamoto za Mahkama ya Ardhi

a) Mahakama ya Ardhi bado inakabiliwa na changamoto ya uingizwaji wa fedha jambo ambalo linakwaza kutotekelezeka kwa shughuli ambazo imejipangia katika mpangokazi wake.

MAAGIZO, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1. Kamati inaendelea kuisisitiza Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kulitafutia ufumbuzi suala la upatikanaji wa fedha kwa Mahkama ya Ardhi ili waweze kutekeleza majukumu yao waliyopangiwa.
2. Kamati inaishauri Mahkama ya Ardhi kuendelea kujikita katika matumizi ya njia ya usuluhishi wa kutatua migogoro ili kuwapunguzia wananchi gharama na muda wa kufuatilia mashauri Mahkamani.

3:2:3 OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI.

Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ina jukumu la usimamizi mzuri wa uthaminishaji rasilimali kwa malengo mbali mbali ya Sekta ya Umma, Biashara na Wananchi kwa ujumla. Kamati ilipoonana na watendaji wa Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ilibaini kwamba

kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imetekeleza shughuli mbali mbali ikiwemo: -

(i) Jumla ya ripoti 231 zimethibitishwa na Mthamini Mkuu ambapo kati ya hizo, 48 ni ripoti za Fidia (Taasisi-COLA, WAMM, ZECO, MOIC, ZHC).

(ii) Imetayarisha viwango vya uthamini ambapo Rasimu ya muongozo wa Uthamini wa mali na Malipo ya fidia umewasilishwa kwa Kamati ya Makatibu Wakuu na kutoa marekebisho yao ambayo yamefanyiwa kazi.

(iii) Imehifadhi Ripoti 231 katika mfumo wa Ms Excel kwa lengo la kutunza kumbukumbu za taarifa zote za uthamini zilizofanywa. Ofisi hii kwa sasa haina Mfumo wa kieletriniki kwa ajili uwekaji wa kumbukumbu wa kazi za Uthamini.

Changamoto za Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali.

a) Uhaba wa upatikanaji wa fedha za kuendesha Ofisi. Ambapo Ofisi kwa sasa imekodi jengo la Michenzani Mall ambapo inashindwa kulipa kodi ya jengo hilo kwa wakati kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha za kuendesha Ofisi.
b) Uhaba wa vyombo vya usafiri.
c) Kuendelea kukosekana kwa mfumo wa kisasa (kidigitali) wa kuhifadhia taarifa na ripoti za uthamini zinazofanywa na Ofisi**.**

MAAGIZO, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Kamati inaendelea kuisisitiza Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kutekeleza Miradi inayoletwa kupitia Taasisi mbali mbali kwa haraka ili kuzuia Miradi kuchelewa kuanza utekelezaji.
2) Kamati bado inaishauri Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kupitia vizuri tathmini zao ili kupunguza lawama kwa wananchi wasioridhika na tathmini ya maeneo yao.
3) Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ipatiwe nguvu ya rasilimali fedha pamoja na rasilimali watu ili iweze kufanya kazi zake kwa uweledi.

3:3 SEKTA YA MAKAAZI

Taasisi zinazounda Sekta hii ni Idara ya Maendeleo ya Makaazi, Shirika la Nyumba na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba ambapo jukumu la Sekta hii ni kuhakikisha upatikanaji wa Makaazi salama na endelevu kwa wananchi pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa sekta binfsi katika huduma za makaazi.

3:3:1 IDARA YA MAENDELEO YA MAKAAZI

Jukumu la kusimamia suala la Makaazi na kusajili, kuratibu matumizi pamoja na majengo yenye sehemu zinazomilikiwa na watu tofauti, ikiwemo majengo ya ghorofa linasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi. Hadi Disemba, 2024, Idara ya Maendeleo ya Makaazi imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Inaendelea na hatua za usajili wa Kondominio kwa Unguja na Pemba ambapo Ofisi imetoa jumla ya fomu Mia Moja na hamsini (150) za maombi mbalimbali ya usajili wa Kondominio.

(ii) Imefanya usajili wa Ramani Sita (6) katika miradi ya Kondominio.

(iii) Imeendelea kufanya uchambuzi na kuhakiki maombi 131 ya usajili.

(iv) Imeendelea na zoezi la utoaji wa elimu kuhusu usajili wa fleti za Kondomino uanzishwaji wa Jumuiya za Kondominio kwa wamiliki na wakaazi wa Nyumba za Maendeleo Wete – Pemba.

(v) Imeshirikiana na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kuandaa Sera ya Maendeleo ya Miji na Makaazi ambayo kwa sasa ipo katika hatua ya kuwasilishwa katika kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu baada ya kuingizwa maoni ya wadau.

Changamoto za Idara ya Maendeleo ya Makaazi

a) Kuendelea kukosekana kwa vitendea kazi ikiwemo usafiri wa ufuatiliaji wa Miradi ya Kondominio.
b) Mazingira ya Nyumba zilizopo chini ya Kondomino bado hayaridhishi.

MAAGIZO, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Bado Kamati inaendelea kuishauri Wizara kuwasiliana na kila Taasisi yenye Miradi ya Kondominio kuhakikisha inafuata taratibu za usajili wa Kondominio kwa mujibu wa Sheria.
2) Idara iendelee kutoa elimu ya uhamasishaji kuhusu usafi wa mazingira na faida ya kutunza na kuimarisha mandhari ya nyumba hizo.

3:3:2 SHIRIKA LA NYUMBA

Shirika limepewa mamlaka ya kusimamia na kuendeleza Sekta ya nyumba Zanzibar kwa lengo la kuongeza pato la Taifa na kuwapatia wananchi makaazi bora na endelevu.

MAFANIKIO YA SHIRIKA LA NYUMBA

Kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2024 miongoni mwa mafanikio ya Shirika ni kama yafuatayo: -

(i) Ujenzi wa majengo manne yenye nyumba 72 za Makaazi na maeneo ya biashara Mombasa (Kwa Mchina) yamekamilika na kufunguliwa rasmi. Shirika tayari limeshaanza kukabidhi nyumba kwa wateja waliomaliza malipo ya nyumba hizo kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa.

(ii) Ujenzi wa jengo nambari 1293/1294 la Darajani lenye ghorofa tatu umekamilika na kufunguliwa rasmi.

(iii) Matengenezo ya Jengo namba 1699/1705 Mkunazini (Mnadani) awamu ya pili 'A' inayohusisha maduka manne na nyumba tano imekamilika. Aidha, kazi zinazoendelea ni kufunga ringbeam za juu kwa ajili ya kumwaga zege 'slab' katika awamu ya pili 'B'.

(iv) Ujenzi wa jengo la ghorofa nne la biashara na makaazi Mkungu Malofa (Mabatini) Chake chake - Pemba unaohusisha nyumba nne za makaazi na maduka ishirini umekamilika na kufunguliwa.

(v) Ujenzi wa jengo la ghorofa tatu Machomane Pemba unaendelea kwa hatua ya ujenzi wa nguzo pamoja na formwork ya lifti. Ujenzi huu awali ilikuwa ni kwa matumizi ya ofisi ambapo kwa sasa utakuwa ni makaazi kwa ajili ya mahitaji yaliyopo.

Changamoto za Shirika la Nyumba

a) Uchakavu wa nyumba za Shirika hasa zile za Mji Mkongwe kutokana na kukaa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo.
b) Hali mbaya na matumizi yasisyo sahihi katika nyumba za Maendeleo Mijini na Vijijini.
c) Kutokukidhi mahitaji ya nyumba na makaazi kwa Zanzibar kwa kuwa mahitaji halisi ya nyumba kwa sasa ni makubwa mno kulingana na uwezo mdogo wa Shirika wa kuweza kukidhi mahitaji hayo.
d) Uwepo wa deni kubwa na la muda mrefu la wapangaji wa nyumba za Shirika.
e) Nyumba zinazojengwa na Shirika ni za bei ya juu, hali inayopelekea wananchi wengi kutomudu kuzinunua.

MAAGIZO, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Kamati inaiomba Serikali kupitia Shirika la Nyumba kuangalia uwezekano wa kuzihami nyumba zake za Mji Mkongwe ili kujikinga na athari au hasara inayoweza kutokea hapo baadae.
2) Kamati inalishauri Shirika la Nyumba lifikirie wazo la kuangalia upya bei za Nyumba mpya wanazojenga kulingana na uhalisia wa vipato vya wananchi ili wananchi wengi waweze kumudu kununua nyumba hizo.
3) Kamati bado inalilisisitiza Shirika kubuni njia mpya za uhamasishaji kwa wateja waliopanga katika nyumba za Shirka ili wawe na moyo wa kusawazisha madeni yao kwa hiari.

WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI

4:0 MUUNDO WA WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI

Wizara ya Maji, Nishati na Madini inaundwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Maendeleo ya Maji, Idara ya Nishati na Madini pamoja na Afisi Kuu – Pemba. Aidha, Wizara hii ina Taasisi tatu ambazo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati - Zanzibar (ZURA), Mamlaka ya Maji - Zanzibar (ZAWA) na Shirika la Umeme - Zanzibar (ZECO).

4:1 MALENGO YA WIZARA

Lengo kuu la Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutoa huduma nafuu, endelevu na zilizo bora kwa wananchi wote katika mazingira yanayofaa kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma za maji, nishati na madini.

4:2 IDARA YA MAENDELEO YA MAJI

Idara ya Maendeleo ya Maji ina jukumu la kusimamia masuala yanayohusu sekta ya maji nchini. Kamati imeelezwa kwamba katika kipindi cha Julai – Disemba, 2024. Idara hii imeandaa ramani ya miundombinu mikongwe ya mabomba ya mtandao wa maji safi na salama katika Mkoa wa mjini Magharibi, ambapo itawezesha kuweka kumbukumbu bora na kutatua changamoto zinazoweza kujitokeza na pia kuepusha uharibifu wa miundombinu wakati wa ujenzi wa barabara na shughuli nyengine.

Kwa Upande mwengine, Kamati imearifiwa kuhusu taarifa za kuchukua hatua ya kuunganisha huduma ya maji baada ya kuona kasi ya uunganishwaji kupitia mradi wa Exim- India haikuwa ya kuridhisha. Jumla ya nyumba 2,720 zimeunganishwa na huduma ya maji ikiwemo Skimu ya Mkorogo (393), Skimu ya Maungani (758) na Mfenesini (1,569) kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi.

4:3 MAMLAKA YA MAJI - ZANZIBAR (ZAWA)

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imeanzishwa chini ya Sheria Namba 4 ya Mwaka 2006 kama ilivyopendekezwa katika Sera ya Maji ya Taifa ya Zanzibar ya Mwaka 2004, ikiwa na jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na kulinda na kuhifadhi rasilimali maji kwa watumiaji.

Hali Halisi ya Uzalishaji wa Maji

Hadi kufikia Disemba 2024 kasi ya uzalishaji wa maji safi na salama umeongezeka kwa kupitia visima 393 ambavyo kwa Unguja ni visima 242 vinavyozalisha maji na Pemba ni visima 151. Hali iliyopelekea uzalishaji wa maji Zanzibar kufikia wastani wa asilimia 83.47 (kwa Unguja Asilimia 85.57 na Pemba ni asilimia 80) ambapo mahitaji ni Lita **275,980,481** kwa siku, uzalishaji ni lita **230,369,094** kwa siku, na mapungufu ni lita **45,611,387.**

Jadweli 10: Mahitaji, uzalishaji pamoja na mapungufu kwa Unguja na Pemba

NA	MKOA	Mahitaji ya maji (lita kwa siku)	Uzalishaji wa maji (Lita kwa siku)	Mapungufu (Lita kwa siku)	Asilimia ya uzalishaji (%)
1.	Mjini Magharibi	125,043,660	108,435,600	16,608,000	86.72
2.	Kaskazini Unguja	36,020,600	21,394,800	14,625,800	59.40
3.	Kusini Unguja	27,422,220	30,328,200	+2,905,980	110.60
4.	Kaskazini Pemba	43,806,651	31,718,534	18,352,904	72.41
5.	Kusini Pemba	43,687,350	38,491,960	12,842,550	88.1
	JUMLA KUU	**275,980,481**	**230,369,094**	**45,611,387**	**83.47**

Chanzo: ZAWA,2024

Hali Halisi ya Upotevu wa Maji

Kamati imeendelea kubaini kuwepo kwa jitihada za kuzuia upotevu wa maji unaotokana na kupasuka kwa mabomba ya maji. Kuna jumla ya mivujo 1,188 kwa Zanzibar ambapo 508 ni Unguja na 680 ni upande wa Pemba. Kadhalika, ZAWA bado inaendelea kubadilisha mabomba chakavu na kulaza mabomba mapya ambayo kwa kiasi kikubwa itapunguza idadi

ya mivujo na upotevu wa maji ili maji mengi zaidi yanayozalishwa yaweze kuwafikia wananchi kama ilivyokusudiwa.

Hali ya Madeni ya Wateja wa ZAWA

Mamlaka ya Maji – Zanzibar ina jumla ya wateja 135,806 waliojigawa katika makundi mbali mbali. Kamati imebaini kwamba hadi kufikia Disemba, 2024/2025 ZAWA ilikuwa inadai jumla ya **TZS Bilioni 2,815,918,107.18** kutoka kwa wateja wake Unguja na Pemba kama inavyoonekana katika jedweli lifuatalo; -

Jadweli 11: Madeni ya wateja wa ZAWA hadi Disemba, 2024.

NAM.	AINA YA WATEJA	IDADI	DENI
i.	Wateja wa Majumbani	**132,375**	2,259,576,570.66
ii.	Wateja wa Biashara	**1,405**	367,741,261.40
iii.	Wateja wa Taasisi	**1,712**	161,851,446.49
iv.	Wateja wa kilimo	**297**	17,297,328.63
v.	Wateje wa Viosk	**17**	9,451,500.00
JUMLA		**135,806**	**2,815,918,107.18**

Chanzo: ZAWA, 2024

Changamoto zinazoikabili ZAWA

Katika kutekeleza majukumu yake Kamati imeona bado ZAWA inakabiliwa na changamoto mbali mbali zinazopelekea kupunguza kasi ya utekelezaji na ufanisi wa kazi zikiwemo: -

a) Idadi kubwa ya wateja wasiokuwa na mita za maji.

b) Kamati imebaini kuna tatizo la ufungaji wa mita katika baadhi ya mitaa, hali inayopelekea kuvujisha maji kwa wingi na kuharibu mandhari ya mazingira mitaani.

c) ZAWA bado inaendelea kukumbwa na tatizo la Uhaba wa wataalamu katika fani za Uhandisi.

d) Kupanda na kushuka kwa umeme mara kwa mara kunakopelekea hitilafu za kuungua pampu na vifaa katika visima.

e) Uharibifu wa mtandao wa maji kutokana na ujenzi wa Barabara katika sehemu mbali mbali.

f) Uwepo wa miundombinu chakavu ya maji hususan bomba za Asbestos cement (AC) na uPVC.

g) Kuendelea kukosekana kwa hatimiliki katika maeneo ya vianzio vya maji.

h) Uvamizi wa maeneo ya vianzio vya maji pamoja na hujuma za miundombinu ya maji.

i) Kukosekana kwa takwimu, utambuzi pamoja na wamiliki wa visima binafsi vya maji.

j) Uwepo wa madeni makubwa kwa wateja wa maji.

k) Deni kubwa la fidia za wananchi, lililofikia TZS 16,471,413,790.30 hadi Disemba, 2024.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Kamati bado inasisitiza na kuiomba ZAWA kushirikiana na Wizara kuendelea kuomba wataalamu kupitia OR - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ili kuweza kukidhi mahitaji na kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi za kila siku za Mamlaka.

2) Kwa mara nyengine tena, Kamati inaendelea kuhimiza kuyahifadhi maeneo ya vianzio vya maji kwa kujenga uzio, kupanda miti mbalimbali, kutafuta hatimiliki na kuweka ulinzi ulio imara.

3) Kamati inapendekeza ZAWA kuharakisha ufungaji wa vifaa maalum vya kudhibiti ongezeko la umeme pamoja na kufunga umeme wa jua (solar power) ili kuepusha uunguaji wa pampu na vifaa mara kwa mara na kupunguza gharama za kulipia umeme katika shughuli za uendeshaji.

4) Kamati inasisitiza jitihada za ziada zizidi kuchukuliwa kwenye suala la utambuzi wa mfumo wa mtandao wa maji wa ZAWA ikiwa ni njia moja wapo ya kuulinda na kuepukana na uharibifu wa mara kwa mara unaojitokeza.

5) Kamati inashauri kuwekwa utaratibu mzuri wa kitakwimu utakaowezesha kuwatambua wamiliki na idadi ya visima pamoja na kupatiwa dawa za kutibu maji ili kupunguza matumizi ya maji yasiyo salama na kuepusha mripuko wa maradhi katika jamii.

6) Kamati pia inaishauri ZAWA kuwa kuna baadhi ya visima na matangi ya maji kwa Unguja na Pemba havina tija kwa wananchi, hivyo, ni jukumu la ZAWA kuvitambua visima pamoja na matangi na kuchukua hatua muafaka kwa kuviondosha kabisa au kufanya ukarabati vikaweza kutumika ili kuongeza uzalishaji na uunganishwaji wa maji majumbani na hatimaye kuongeza huduma kwa wananchi.

7) Kamati inaiomba ZAWA kufuatilia yaTume ya Mipango maombi ya fidia kwa wananchi waliopisha Miradi ya ZAWA ili kuondosha mkanganyiko unaojitokeza kwa wananchi hao.

4:4 IDARA YA NISHATI NA MADINI

Idara ya Nishati na Madini ni moja kati ya Idara za Wizara ya Maji, Nishati na Madini ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia masuala yote yanayohusiana na Nishati na Madini. Idara imejigawa katika sekta ya Nishati na Sekta ya Madini.

4:4:1 Sekta ya Nishati

Sekta hii inajishughulisha na uratibu wa masuala yote ya nishati ikiwemo nishati mbadala, nishati ya kisasa, mafuta, gesi asilia, umeme pamoja na kutoa elimu juu ya matumizi ya nishati kwa jamii, taasisi za Serikali na zisizo za Serikali.

Baadhi ya Mafanikio katika Sekta ya Nishati

Katika kipindi hiki cha Tathmini na ufuatiliaji, Kamati imebaini yafuatayo; -

(i) Idara imetoa elimu kuhusu matumizi ya nishati za kisasa na nishati mbadala kupitia maonyesho ya kilimo ya nanenane na Tamasha la Kizimkazi.

(ii) Kutangaza zabuni ya dharura ya uzalishaji wa umeme wa megawati 50 kwa Zanzibar ambapo jumla ya Kampuni sita (6) ziliwasilisha maombi na Kampuni ya Karpowership kutoka Uturuki ilifanikiwa kupata tenda hiyo kwa ajili ya utekelezaji.

Changamoto katika Sekta ya Nishati

a) Mwiitikio mdogo wa Wawekezaji wenye nia ya kuekeza katika miradi ya umeme wa upepo, jua na mawimbi.

b) Kuendelea kutokuwepo kwa Sheria ya Nishati ambayo ndiyo nyenzo kuu kwa Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini itayowezesha kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuzisimamia moja kwa moja Taasisi zilizopo chini ya Wizara, jambo ambalo linapelekea Taasisi hizo kufanya baadhi ya maamuzi bila ya Wizara kuwa na taarifa.

c) Kupitwa na wakati kwa Sera ya Nishati ya mwaka 2009.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Kamati bado inaendelea kuishauri Wizara Kupitia Idara ya Nishati a Madini kuwasiliana na wadau wa maendeleo ili kuzidi kusaidia kuupitia tena utafiti wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo ili utekelezaji wake ukidhi haja ya mahitaji ya wananchi.

2) Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kukamilisha mapitio ya Sera ya Nishati ya 2009, ambayo kukamilika kwake kutaiwezesha Wizara kuendelea na mchakato wa kuandaa Sheria ya Nishati.

4:4:2 Sekta ya Madini

Sekta hii inajishughulisha na uratibu wa masuala ya madini ikiwemo Maliasili Zisizorejesheka, uthaminishaji wa madini yanayoingia na kutoka nchini kwa lengo la kuhakikisha Serikali inapata mgao wake stahiki, pamoja na uratibu wa masuala mbalimbali ya kijiolojia.

Mafanikio Katika Sekta ya Madini

(i) Imepokea na kufanyia kazi Jumla ya maombi 764 ya leseni za kusafirisha Maliasili Zisizorejesheka pamoja na kupima gari kwa kutumia mzani wenye kuhamishika.

(ii) Kufanya doria katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar pamoja na kufanya maboresho ya kikosi cha doria mara kwa mara, ili kuongeza ufanisi kazini. Zanzibar.

(iii) Kufanya utafiti wa miamba na kuandaa ripoti ya jiolojia ya Zanzibar iliyoambatana na ramani ya kijiolojia. Uzinduzi wa ripoti hiyo umefungua sura mpya ya uwekezaji katika sekta ya madini Zanzibar.

Changamoto katika Sekta ya Madini

Changamoto zinazoikabili sekta ya madini ni kama zifuatazo: -

a) Baadhi ya gari zinazotumika katika utekelezaji wa miradi ya Serikali ikiwemo ya barabara kuendelea kuuza kifusi kwa wananchi, hali hii inapelekea kupotea kwa mapato
b) Wananchi kutofuata vipimo vya upakizi vilivyowekwa katika gari za usafirishaji Maliasili Zisizorejesheka.
c) Kuendelea kuripotiwa kwa vitendo vya uchimbaji holela wa maliasili zisizorejesheka.
d) Magari ya Kampuni zinazotekeleza miradi ya Serikali kutowalishwa kwa ajili ya upimaji licha ya kupatiwa barua za ukumbusho.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Kamati inaendelea kuiomba Wizara kuwasiliana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili iwasimamia vyema wakandarasi ambao ndio wamiliki wa gari zinazotumika kusafirisha Maliasili Zisizorejesheka katika maeneo ya miradi pamoja na kuzichukulia hatua za kisheria gari zinazobainika kufanya makosa hayo.
2) Kamati inaendelea kuishauri Wizara kuendelea na doria pamoja na kuimarisha kikosi cha doria kwa kuomba askari wa ziada kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ili kuweza kukabiliana kikamilifu na uchimbaji holela wa Maliasili Zisizorejesheka.
3) Wizara iendelee kuzikumbusha Taasisi za Serikali juu ya kufuata utaratibu wa uchimbaji na usafirishaji wa Maliasili Zisizorejesheka ili kuepuka usumbufu wakati wa utekelezaji wa miradi yao.
4) Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kupitia idara ya Nishati na Madini kutafuta utaratibu mzuri wa kupata usimamizi wa maeneo yanayohuishwa, ili uhuishaji huo uweze kuwa na matokeo Chanya.

4:5 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)

Shirika la Umeme Zanzibar linajukumu la kuwezesha uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na uuzaji wa Umeme Zanzibar.

4:5 :1 Hali ya Miundombinu ya Umeme Unguja na Pemba

Visiwa vya Unguja na Pemba vinapata umeme kupitia waya za baharini zenye uwezo wa Megawati 100 na Megawati 45 za mkondo wa Kilovoti 132 kwa upande wa Unguja na Megawati 20 za Mkondo wa Kilovoti 33 kwa upande wa Pemba kutoka Gridi ya Taifa ya Tanzania Bara.

Miundombinu ya umeme Zanzibar imegawika katika makundi makuu mawili. Line za kilovoti 33 ambazo zinakwenda masafa marefu na line za kilovoti 11 ambazo ni za masafa mafupi. Kwa upande wa line za kilovoti 33 jumla zipo line sita (6) na line za kilovoti 11 zipo Kumi (10).

4:5 :2 Matumizi ya Umeme Zanzibar kwa sasa

Hali halisi ya miundombinu ya umeme kwa sasa imefikia kiwango cha Asilimia 94 cha matumizi, ambapo baadhi ya line za 33 kilovoti zimefikia kiwango cha Asilimia 99 cha matumizi na kupelekea kuzima zima kwa umeme, mfano line inayopeleka umeme Nungwi na line ya Kizimkazi, Paje na Jambiani.

Aidha, Kamati imebaini kuwa kutokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi ndani ya visiwa vya Zanzibar matumizi ya umeme yameendelea kukua na kuongezeka ambapo kiwango cha juu cha matumizi ya umeme kilichofikiwa ni 92.50 Megawati sawa na Asilimia 92.5 kwa upande wa njia mpya ya Megawati 100, na kwenye line kongwe kiwango cha juu kilichofikiwa ni 37.60 megawati sawa na Asilimia 83.7.

4:5 :3 Mafakikio ya ZECO Kuanzia Julai – Disemba, 2024

Kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Maji, Nishati na Madini katika kipindi hiki cha ufuatiliaji ZECO imepata mafanikio kadhaa ikiwemo: -

(i) Kupeleka huduma ya umeme katika vijiji 24 (19 Unguja na 5 Pemba), sawa na asilimia 80 ya lengo la vijiji 30 (18 Unguja na 12 Pemba).

(ii) Shirika lilipanga kutumia TZS. 12.3 Bilioni kwa uimarishaji wa miundombinu ya umeme. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kubadilisha nguzo mbovu 937 (601 Unguja na 336 Pemba) na kusawazisha maeneo 22 yenye umeme mdogo, sawa na asilimia 100 ya maeneo yaliyopangwa,

(iii) Shirika limefanya ukaguzi wa transfoma 523 (Unguja 375 na Pemba 148), sawa na asilimia 55 ya transfoma 959 zilizopangwa kukaguliwa. Transfoma 44 zilizopo Unguja zilibainika kuwa na matatizo na zimefanyiwa marekebisho.

(iv) Shirika limewaunganishia huduma ya umeme wateja wapya 15,378 (13,246 Unguja na 2,132 Pemba), sawa na asilimia 80 ya lengo la wateja 19,200 (15,600 Unguja na 3,600 Pemba).

Hali ya Madeni ya Wateja wa ZECO

Kamati imebaini kwamba katika utekelezaji wa majukumu yake, Shirika la Umeme Zanzibar limekuwa likikabiliana na changamoto mbali mbali ikiwemo ya ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wateja wake. Hadi Disemba 2024, Shirika linawadai wateja wake Unguja na Pemba jumla ya **TZS. Bilioni 69,306,442,425.9** ambapo mchanganuo ni kama ifuatavyo; -

Jadweli 12: Madeni ya wateja wa Umeme hadi Disemba 2024.

Maelezo	Unguja	Pemba	Jumla
SMZ-ZAWA	27,076,521,981.04	25,025,762,546.39	**52,102,284,527.43**
SMZ - NYENGINEZO	7,334,193,148.04	27,273,938.96	**7,361,467,087**
JWTZ	2,093,904,162.59	546,749,541.4	**2,640,653,703.99**
SMT - NYENGINE	184,182,388.81	0.0	**184,182,388.81**
WATEJA BINAFSI	6,991,488,263.07	26,366,455.6	**7,017,854,718.67**
JUMLA KUU	**43,680,289,943.55**	**25,626,152,482.35**	**69,306,442,425.9**

Chanzo: ZECO, 2024

Ziara ya Kamati katika Vituo vya kuleta na Kupokelea Umeme

Katika kufuatilia utendaji na ukaguzi wa Mioundombinu ya ZECO, Kamati ilitembelea Vituo vikuu vya Kuleta na Kupokea Umeme kutoka Tanzania Bara ambapo kwa Pemba ni Mnyanjani Tanga na Ras Mkumbuu pamoja na Wesha na Unguja ni Ras Kiromoni Dar es Salaam na Fumba pamoja na Mtoni. Miongoni mwa Changamoto zilizobainika na kamati ni kama zifuatazo: -

a) Kutokuwepo kwa Kifaa cha akiba cha kupimia mafuta mazito yanayotumika kulainisha mzunguko wa waya wa zamani ambao pia uko katika mfumo wa zamani.

b) Kamati imebaini uwepo wa changamoto kadhaa katika kituo cha kupokelea umeme Wesha zizazotokana na ukosefu wa maji safi na salama, uchakavu wa jengo na vifaa, uhaba wa wafanyakazi mazingira ya kazi yasiyoridhisha

pamoja na mawasiliano yasiyo rafiki kati ya kituo hicho na kile cha Majani Mapana Tanga hasa pindi khitilafu ikitokea.

c) Ukosefu waa maji pamoja na banda la kukaa kwa askari wanaolinda kituo cha kupokelea umeme cha Ras Mkumbuu kinachopokea umeme kutoka Tanga hadi Pemba.

d) Kituo cha Mnyanjani Tanga hakipo kwenye mazingira mazuri ya kiusalama pamoja na kupotea baadhi ya alama zilizowekwa za kuonesha maeneo yaliyopita umeme kuelekea baharini.

e) Uwepo wa vifaa vingi vya umeme vya mfumo wa zamani kwa Pemba ambavyo vimeharibika na havitengenezeki tena wala kutumika.

Changamoto nyengine za Jumla za ZECO zilizoibuliwa na Kamati ni pamoja na: -

f) Kuendelea kwa utaratibu usioepukika wa matumizi ya umeme kabla ya malipo.

g) Kuendelea kwa uwepo wa malimbikizo ya madeni kwa wateja wa Shirika la Umeme unatokana na baadhi ya wateja kushindwa kulipa ankara zao za matumizi ya umeme kwa ukamilifu na kwa wakati.

h) Uhaba wa gari za kisasa za kuchukulia na kunyanyulia nguzo ambapo kwa sasa ZECO imejielekeza kuweka nguzo za zege zinazohitaji teknolojia katika uwekaji wake.

i) Ukosefu wa ukarimu wakati wa kutoa huduma (*Customer care)* ambapo baadhi ya watendaji hutoa majibu yasiyoridhisha kwa wateja na kupelekea wananchi kukosa imani wakati wanapohitaji huduma.

j) Kamati imebaini kutoendelezwa kwa vijana wazalendo waliolitumikia shirika kwa kufanya kazi katika maeneo ya visiwa mbalimbali.

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Shirika na Wizara kwa ujumla iendelee kufanya mazungumzo na Taasisi za Serikali (SMZ na SMT) kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Zanzibar, ili kusawazisha madeni yaliyopo pamoja na kufanya malipo ipasavyo kwa mujibu wa matumizi yao ya umeme ya kila mwezi kwa taasisi hizo.
2) Kamati inasisitiza kwa Wizara kupitia ZECO kuongeze bidii ya utoaji wa elimu kwa umma juu ya madhara na athari zinazotokana na uvamizi, wizi na uharibifu wa miundombinu ya umeme.

3) Kamati inashauri zoezi la uwekaji wa nguzo za zege katika maeneo tofauti ikiwemo maeneo ya barabara ya kisakasaka liwe endelevu na ni vyema ikatafutwa rangi maalum zikapakwa nguzo hizo ili kuweka mandhari yetu yawe ya kipekee na yenye kuvutia.

4) Kamati bado inapendekeza elimu ya utoaji huduma bora kwa wateja iwe inatolewa mara kwa mara hasa kwa watendaji wanaohusika na Wizara hii ya Maji, Nishati na Madini ili waweze kushirikiana kwa pamoja kutoa huduma nzuri na zenye tija kwa wananchi.
5) Kamati inaishauri ZECO kuwa na utaratibu maalum wa kuangalia uwezekano wa kuajiri vijana wanaoishi ndani ya Visiwa vyevyewe ili kurahisisha utoaji wa huduma ya umeme pale haja inapohitajika.
6) Kamati inapendekeza kitafutwe mapema kifaa chengine cha kupimia mafuta mazito katika kituo cha Fumba ili pindipo kikipata khitilafu yoyote kuwe na mbadala wake ili kuengeza ufanisi wa uendeshaji.
7) Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utaratibu wa kutafuta magari ya kisasa yenye teknolojia ya kuchukua nguzo nzito za zege au chuma kuweza kuinulia na kuzipachika kwa wepesi zaidi.
8) Kamati inaishauri ZECO kuzidi kuwachukulia hatua mafundi wanaojishughulisha na hujuma za umeme ikiwemo umeme unaopotea kwa ***by pass*** ambapo takriban mega wati 20 zinapotea kwa njia hiyo.

9) Kamati inaishauri Serikali kupitia wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kufanya utafiti wa kina kwa watendaji wa Vituo vya Kupokelea Umeme ili kubaini athari za kiafya, kiakili na kimwili zilizozunguka mazingira ya utendaji kazi wao pamoja na unyeti wa kazi zao kwa nchi ukilinganisha na maslahi wanayopewa.
10) Kamati pia inashauri kuweka utaratibu maalum na wa haraka wa kutengeneza na kurekebisha vituo vyote vya umeme pamoja na kuwapatia usafiri ili wafanyakazi wawe na ari na hamu zaidi ya kufanyakazi tukitambua kwamba mazingira mazuri ya kazi huongeza ufanisi**. (Conducive Environment Direct Proportional to the Efficiency)**
11) Kamati pia inasisitiza jitihada za uharaka zizidi kuchukuliwa zinazolenga kuzalisha umeme wa Meli (Powership) ambao utaelekezwa kwenye laini ya kaskazini ambako kuna tatizo kubwa la umeme.

MAONI YA WADAU WA SEKTA YA UMEME

Kamati ilipata fursa ya kuzungumza na wadau wakiwemo taasisi binafsi, Baraza la Ushindani wa Kibiashara, ZATI na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kuhusu hali ya umeme katika nchi yetu na kutoa maoni yafuatayo: -

a) Kuwe na generata za diseli ambazo zitazopunguzwa ushuru ili mtu binafsi aweze kumudu kuzalisha umeme wake.
b) Serikali iwawezeshe wadau mbali mbali kuingia katika uzalishaji wa umeme na endapo mdau atakuwa na uwezo wa kuzalisha kiwango kikubwa zaidi ya mahitaji yake aruhusiwe kuuingiza katika gredi kubwa ili kutumiwa na wananchi.
c) Serikali ijikite pia kwenye uzalishaji wa umeme mbadala kama vile umeme unaotokana na mawimbi, jua na upepo.

4:6 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI (ZURA)

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar – ZURA ilianzishwa kwa Sheria Namba 7 ya mwaka 2013, majukumu yake ni kudhibiti huduma za maji na nishati ya mafuta, gesi na umeme, ili kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa kiwango bora.

Udhibiti wa Huduma za Maji

Kwa kipindi hiki, ZURA ilifanya ukaguzi katika wilaya ya Magharibi 'A', Kaskazini "A" na "B" pamoja na kusini. Jumla ya visima Arobaini na Moja (41) vinavyotumika kuzalisha maji pamoja na miundombinu yake ilikaguliwa, matokeo ya ukaguzi wa awali katika wilaya ya Kaskazini "B" yamebainisha kuwa baadhi ya changamoto zilizogundulika katika visima vinne (4) zimeshafanyiwa kazi (visima vya Donge Bandamaji, Kidanzini, Kisongoni Kongwe na Kitope skuli).

Aidha, ukaguzi wa Magharibi "A" umebaini kati ya hivyo visima Ishirini na Tisa (29) ambapo visima 20 vinafanya kazi na Tisa (9) havifanyi kazi kutokana na sababu za kuharibika kwa Pump na hitilafu za Control Pannel za kuwashia.

Jadweli 13: Wilaya zilizofanyika ukaguzi

Wilaya	**Idadi ya visima/vituo vilivyokaguliwa ubora wa maji**
Kaskazini 'B'	10
Magharibi 'B'	17
Kusini	7
Magharibi 'A'	7
Jumla	**41**

Chanzo: ZURA, 2024

Changamoto zilizobainika katika ukaguzi wa miundombinu na mazingira ya vituo vya uzalishaji maji Unguja ni: -

a) Uwepo wa hitilafu za Control Pannel za kuwashia maji.

b) Kuwepo kwa mazingira yasiyoridhisha katika baadhi ya "Pump House" na miundombinu ya visima zikiwemo "Well Head".

c) Kukosekana vifaa vya dharura wakati wa hatari katika vituo vyote.

d) Kukosekana pampu ya dharura (standby pump).

e) Kukosekana kwa taarifa za kiwango (Ujazo) cha maji yanayozalishwa na kusambazwa.

Changamoto zilizobainika katika ukaguzi wa miundombinu na mazingira ya vituo vya uzalishaji maji Pemba ni: -

Kamati pia ilipokea taarifa ya ZURA kuhusiana na Ukaguzi wa visima kwa upande wa Pemba, ambapo jumla ya visima 50 ambavyo 10 katika wilaya ya Mkoani, Visima 21 katika wilaya ya Chake Chake, Visima 8 katika wilaya ya Wete na visima 11 vya wilaya ya Micheweni. Katika ukaguzi wa ubora wake wa maji katika Wilaya ya Wete, Mkoani na Micheweni yamebainika yafuatayo: -

a) Visima havina uzio kabisa.

b) Visima ambavyo vipo katika hali hatarishi ya ubora wa maji kutokana na kutohifadhiwa vizuri na kufanyika shughuli za kilimo karibu na vyanzo.

c) Visima vimekosa mfuniko wa juu (wellhead)

d) Visima vingi vilivyozungukwa na vichaka na uchafu wa mazingira.

Udhibiti wa Maji Taka (Maji Machafu)

Katika hatua nyengine, Kamati imebaini kwamba ZURA imeanza hatua za kudhibiti maji taka (Maji Machafu), ambapo imeandaa hadidu rejea (*Terms of Reference-TOR*) kwa ajili ya kumtafuta mshauri elekezi kwa ajili ya *Development of Country Sanitation Road Map*. Hata hivyo, mchakato huo bado upo katika hatua ya manunuzi ili kupatikana mshauri elekezi atakaekidhi vigezo kwa ajili ya uandaaji wa *Sanitation Road Map*.

Udhibiti wa Huduma za Umeme

Kwa upande wa udhibiti wa huduma za Umeme, Kamati imejuilishwa kwamba Mamlaka imefanya ukaguzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika Mkoa wa Kusini Unguja (Wilaya ya Kusini na Wilaya ya Kati) pamoja na Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuchagua maeneo tofauti ya njia za kusambazia umeme kwa lengo la kutambua hali halisi ya huduma inayotolewa kwa wananchi, ambapo jumla ya vituo Mia Moja na Tisa (109) vilikaguliwa katika mtandao wa Shirika la umeme.

Kasoro Zilizobainika Kupitia Ukaguzi wa ZURA Katika Maeneo ya ZECO Yaliyoainishwa Hapo Juu ni Kama Zifuatazo: -

a) Ukosefu wa alama za tahadhari.

b) Uchakavu wa miundombinu.

c) Mazingira machafu

d) Matumizi mabaya ya eneo la Shirika.

Aidha, muhtasari wa matokeo ya ukaguzi umeanishwa katika jadweli lifuatalo: -

Jadweli 14: Matokeo ya Ukaguzi 2024/2025

Hali ya Transfoma (Kasoro)	**Idadi**	**Idadi ya Kasoro**	**Asilimia**
Nguzo mbovu za transfoma	63	2	3.17
Lightining Arrestor zilizokatika	63	2	3.17
Transfoma zinazovujisha mafuta	63	1	1.58
Transfoma zinazotumia njia moja ya umeme (single face)	63	0	0.0
Transfoma zilizounganishwa waya wa earthing (loop)	63	40	63.49

Waya wa earthing zilizokatwa	63	7	11.11
Fuzi za umeme mkubwa zilizofungwa kwa fusi waya bila kifaa	63	14	22.22
Fusi za umeme mdogo zilizofungwa moja kwa moja (direct)	63	8	12.69
Waya wa kusambazia umeme katika transfoma sio mazuri	63	4	6.35
Transfoma zilizokosa alama ya tahadhari	63	54	85.71
Miti/Vipando katika eneo la transfoma	63	40	63.49

Chanzo: ZURA 2024

Ukaguzi wa miradi ya Umeme wa Jua.

Mamlaka hii ilifanya ukaguzi katika miradi mbali mbali ya umeme wa jua ambao ulifanyika katika maeneo halisi iliyopo miradi hiyo. Jumla ya miradi mitatu ilikaguliwa na kubainika yafuatayo: -

(i) Mradi wa Hoteli ya Baraza Resort and Spa: Katika mradi huu unaendelea kuzalisha umeme wa 1MV kwenye hali ya kawaida na kupatiwa leseni mpya ya uzalishaji umeme katika eneo la Bwejuu.

(ii) Mradi wa Matemwe Bungalows ZASWI (Z) Limited: Aidha, mradi huu uko katika hatua za awali unaotarajiwa kuzalisha umeme wa 404 Kilowati na kubainika eneo la uwekezaji linakidhi vigezo vya uwekezaji huo.

(iii) Mradi wa Hotel ya Mayai Ocean Resort: Mradi huu pia unatarajiwa kuzalisha umeme wa wastani wa 29.9 Kilowati, ambapo wakaguzi wa miundombinu walibaini panel arobaini (40 Photo Voltage – PV) zimewekwa kwenye paa la jengo lao (Roof

top) kwa kila panel ina wastani wa 730Wh pamoja na Invetor tano (5) zenye uwezo 11 Kilowati kwa kila moja sawa na 55Kilowati

Udhibiti wa Huduma za Mafuta

Mamlaka imefanya ukaguzi wa Bohari saba (7), Sita (6) kwa upande wa Unguja na moja (1) kwa Pemba, pamoja na ukaguzi wa vituo vyote mia moja na kumi na moja (111) vya mafuta, vituo tisiini na moja (91) kwa Unguja na Ishirini (20) kwa Pemba. Ukaguzi huo ulipelekea kituo kimoja (1) cha Mtofaani Station kuendelea kufungiwa kutokana na kutokidhi matakwa ya Kanuni ya Usimamizi wa Vituo vya Mafuta ya mwaka 2022.

Malalamiko ya watumiaji wa huduma za Maji na Nishati.

Mamlaka imefanya Mikutano miwili (2) kwa ajili ya kutatua malalamiko kwa njia ya usuluhishi na pia ilipokea na kuchunguza Malalamiko kupitia maeneo makuu ya Umeme, Mafuta Gesi na Ulipaji wa fidia kwa wananchi wa Mwangapwani, kama inavyoonekana katika Jedweli lifuatalo: -

Jadweli 15: Idadi na Aina ya Malalamiko yaliyopokelewa ZURA na kushughulikiwa.

Na	Aina	Maelezo	Hatua iliofikia
1.	UMEME	Ajali ya moto kwa watoto (Mahonda)	Hatua ya ununuzi wa Pikipiki umekamilika.
		Kupita kwa miundombinu katika nyumba yake (Karakana)	Lipo katika hatua ya kusubiri majibu kutoka ZECO
		Kuunguliwa kwa Nyumba (Mtambile)	Lipo katika hatua ya kusubiri Ripoti ya Kitaalamu na Kufanya Usuluhishi.
		Kuunguliwa kwa Nyumba (Kijitoupele)	Lipo katika hatua ya kusubiri Ripoti ya Kitaalamu na Kufanya Usuluhishi.
		Kuunguliwa kwa Nyumba (Ziwani)	Lipo katika hatua ya kusubiri Ripoti ya Kitaalamu na Kufanya Usuluhishi.
2.	MAFUTA	Kuwekwa kifusi katika eneo la ujenzi wa Bohari ya UP Mangapwani	Lipo katika hatua ya kusubiri jibu kutoka Wizara ya Mawasiliano
	MAJI	Kuongezwa kwa bei ya Maji katika Kampuni ya Drop of Zanzibar	Hatua ya Kufanya Usuluhishi Umekamilika.

Chanzo: ZURA 2024

MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI

1) Kamati inaishauri ZURA kuendelea kushirikiana vyema na ZECO pamoja na ZAWA kuhakikisha jitihada zinafanyika za marekebisho ya kasoro zilizojitokeza pamoja na kuzingatia taratibu za kiusalama na ubora wa huduma za umeme na maji yanayosambazwa kwa wananchi.

2) Kamati inaendelea kuiomba ZURA kuendelea kutoa miongozo na maelekezo ya kitaalamu ikiwa ni pamoja na kushirikiana na wataalamu wa ZECO na ZAWA katika kurekebisha dosari zilizobainika.

3) Kamati inaishauri ZURA kuzisimamia vizuri kanuni zilizotungwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu na dhamira za uundwaji wa Mamlaka hii ya kuhakikisha udhibiti wa huduma ya maji na nishati unakuwa imara na wenye viwango bora.

4:7 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Kamati pia ilifuatilia taarifa za utekelezaji wa Miradi mbali mbali inayotendelea kutekelezwa chini ya usimamizi wa wizara hii. Baadhi ya miradi hiyo taarifa zake ni kama zinavyoelezwa hapo chini; -

4:7:1 Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar – Exim 92.18 milion. USD

Mradi huu umekamilika na upo katika hatua za uangalizi kwa muda wa mwaka mmoja ili kutizama ufanisi wa miundombinu na endapo itabainika hitilafu yoyote kuweza kurekebishwa.

4:7:2 Mradi Wa Mabadiliko ya Sekta ya Nishati na Upatikanaji wa Huduma ya Umeme Zanzibar (ZESTA)

Hadi kufikia Disemba, 2024 mradi huu umetekelezwa kama ifuatavyo; -

(i) Uendelezaji wa uzalishaji umeme kwa kutumia nishati jadidifu ya jua (solar pv) na miundombinu ya kuhifadhia umeme (Battery Enegy Strage System, BESS).

(ii) Uimarishaji wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme katika kisiwa cha Unguja na vituo vya kupozea na kutawanya umeme.

(iii) Ufungaji kituo cha uendeshaji (Supervision Control and Data Acquisition – SCADA) wa mifumo ya umeme kwa ajili ya misongo ya umeme wa kilovoti 132, 33 na 11.

(iv) Uboreshaji wa njia ya usambazaji umeme katika Mji Mkongwe (Stone town), uendeshaji wa njia mpya (extension) za misongo ya kilovoti 33 na 11 katika visiwa vya Unguja na Pemba.

(v) Uunganishaji wa mfumo wa utayarishaji wa bili za malipo kwa ZECO (SAP ERP and Hexing AMR Billing System Integration and Customer Data Migration).

(vi) Tathmini ya Fidia kwa waathirika (Resettlement Action Plan) na Mazingira (Environmental and Social Impact Assessment (ESIA) na Fidia.

(vii) Kazi ya Ushauri elekezi ya kuandaa Mpango Jumuishi wa Rasilimali za Umeme (Integration Resource Plan).

(viii) Kazi ya ushauri elekezi ya Tathmini na kuandaa mpango wa ujuzi na mahitaji katika sekta ya Nishati (Sector Skills and Capacity Need Assessment).

(ix) Kazi ya ushauri elekezi kwa Shirika la Kiserikali la Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa RAP.

MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI

1) Kamati inashauri Wizara pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar kuongeza juhudi ya uunganishaji wa maji majumbani na kuendelea kuyasambaza katika maeneo yasiyopita miundombinu ya maji ili kuhakikisha miradi mikubwa iliyokamilika kwa asilimia kubwa iendane na lengo lililokusudiwa la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi.

2) Kamati inaendelea kupendekeza kwa Wizara na Shirika kuwa miradi inayofanywa sasa na Serikali ni mikubwa na inatumia gharama kubwa hivyo, Serikali waisimamie vizuri miradi hiyo ili kuwa endelevu (sustainability).

3) Kamati inashauri wafanyakazi wazalendo wawe pamoja na wafanyakzi wa kigeni ili kuweza kumudu kuendesha miradi hii baada ya kukabidhiwa.

4) Pia, Kamati inasisitiza teknolojia inayokuja na miradi hii iwe ni ya kisasa zaidi na inayoendana na kulenga wakati uliopo na ujao ili kuiepushia Serikali kuingia kwenye gharama zaidi pindipo vifaa vikiharibika kwa kutokuwepo tena kwa teknolojia ya awali liyotumika kutengeza vifaa hivyo.

SEHEMU YA TATU - HITIMISHO

5:0 HITIMISHO

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi inawapongeza kwa dhati Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na viongozi na watendaji wote kwa ujumla wa Wizara zote tatu (3) zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamin wa Wizara hizi pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati ilipokuwa Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Aidha, Kamati inatambua, kuthamini na kushukuru kwa ushirikiano mkubwa iliyoupata kutoka Wizara zote tatu tunazozisimamia kwa kuijengea uwezo Kamati na katika Nyakati tofauti kutupeleka katika ziara ya kimafunzo katika maeneo mbali mbali ndani na nje ya Zanzibar.

Mwisho, Kamati inampongeza kwa dhati Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem, Mkurugenzi wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba ndugu Abdulghani Abdullah Said, Wakurugenzi wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, Mratibu wa Kamati Ndg. Khamis Hamad Haji pamoja na sekretarieti yote ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati yetu kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha Ripoti hii kwa mwaka 2024/2025. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.